

UFUNUO WA YESU KRISTO



Asante sana, Ndugu Neville.

Mwaweza kuketi.

² Ninaamini ilisemwa wakati mmoja, kwamba, “Nilifurahi waliponiambia, “Twendeni nyumbani mwa Bwana.””

³ Sasa, tunasikitika kwamba hatuna nafasi, ama nafasi ya kuketi, kwa wote waliopo, na labda itaendelea kuongezeka hata kwenye juma lilalo, ya watu wanaoingia, wakisikia habari za mkutano huu.

⁴ Lakini sababu ya wakati huu maalum ilikuwa ni kwamba tungeniniii. . . Juu ya moyo wangu Roho Mtakatifu alikuwa ameweka ilani hii ya kusadiki, kwamba, “Kanisa katika siku hizi linapaswa kupata Ujumbe huu.” Kwa sababu, ninaamini ya kwamba ndio Ujumbe ulio muhimu sana wa Biblia, kwa sababu unamfunua Kristo katika Kanisa Lake kwenye wakati huu.

⁵ Basi, hakuna mtu anayeweza kupata imani wala kujua wanalofanya, wala wanakoelekea, isipokuwa wawe na ninii, kitu fulani cha kuwekea msingi mawazo na imani yao. Kwa hiyo, kama Maandiko yametufunulia Kristo katika siku hizi za mwisho, na hali ya wakati, ingetufaa sisi ku—kuyachunguza na kuona mahali tulipo.

⁶ Sasa, tuna—tunasikitika ya kwamba kanisa letu si kubwa zaidi, siku moja tunatumaini kuwa nalo.

⁷ Nazo siku hizi nne zilizopita, hasa, nikiusomea huu kwenye sehemu ya kihistoria ya—ya Kitabu cha Ufunuo, nimekutana na mambo ambayo kamwe sikuwazia kweli yaliwahi kutukia. Na hata limeniletea hi—hisia kwamba, baada ya hizi *Nyakati Saba Za Kanisa*, nikiisha kuzipitia hizo, ningependa kuwa na mfululizo mwingine kama huo wa kuleta “Ka—Kanisa la kweli na kanisa la uongo,” pamoja, na kupitia tu kwenye historia na Maandiko. Kama vile wakati mmoja nilivyojaribu sana, kwenye mahubiri, kuchukua “Mzabibu wa kweli na mzabibu wa uongo,” inayopatikana katika Biblia. Nasi tunaninii. . .

⁸ Tutajaribu kupata viti vichache, wakati nikiwazia juu ya watu wanaojaribu kuketishwa. Nasi tutapata, tutajaribu kupata, viti vingine, kujaribu kuvijaza hivyo vyumba huko nyuma, na nje, na vingine huku, tupate kuwaketisha watu wengine zaidi kidogo wakati wa hizo ibada.

⁹ Sasa, juu ya hili, ningemwomba kila mmoja wenu ambaye kweli anahusika juu ya mambo haya, ange—angekuja kila wakati ambapo tuta—tutalielezea. Wala nisingejitolea, ama kujiwazia. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kujitolea kuninii. . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . Kitabu hiki kikuu

cha Ufunuo wa...[Sehemu tupu kwenye kanda.]...Nyakati Saba za Kanisa. Bali ninamtegemea Mungu kwa uchaji, a—apate kunifunulia mara tu ninapokifikia.

¹⁰ Historia ya kawaida, ambayo ni ya...imetolewa kwa wanahistoria hodari sana niwajuao. Kwenye chumba changu cha kusomea, sasa hivi, nina yapata vitabu vitano ama sita vya maelezo, *Babeli Mbili* cha Hislop, *Kitabu Cha Wafia Imani Cha Foxe*, na vitabu vingine mashuhuri; kama kile cha Baraza Lilitangulia Nikea, yapata vitabu vinne juu ya hayo, karibu kurasa mia nne katika kila kitabu. Na hapo lile Baraza la Nikea, na historia yote tuwezayo. Kwa sababu, nyuma ya jambo hili, kutoka kwenye kanda ya sumaku, tutaandika maelezo juu ya Nyakati Saba za Kanisa, tuitume kote ulimwenguni, tuwezavyo, kwa sababu tuko katika siku za mwisho. Tuko katika wakati wa mwisho.

¹¹ Halikuingia moyoni mwangu sana mpaka kwenye—kwenye ule uchaguzi wa mwisho, ndipo nikaona mahali tulipokuwa. Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kunifunulia, ku—kuwaonya watu, na kuliweka hili. Wala siwezi kulifanya katika ka—kanisa kama hili, vya kutosha. Halafu kama ningaliketi chini na kukiandika tu hicho kitabu...Ninajisikia ya kwamba kama ningalienda mimbarani, nao uvuvio wa Roho Mtakatifu miongoni mwa Wakristo unijilie, kunisaidia, basi ningetosheleza zaidi kukiandika hicho kitabu basi, baada ya mimi kukitoka kwenye kanda, kwa maana hapo tungepata uvuvio wake. Hivyo vitabu, hakika, kwa namna fulani vitanyoshwa kidogo, kwa sababu, humu ndani, tunaingiza vitu ambavyo tusingeweza kuviweka kwenye kitabu. Halafu basi sisi...Tena tunachukua muda mwingi kupita kiasi tukijirudia wenyewe, ama ninajirudia. Halafu basi, katika hicho kitabu, yote yatanyoshwa. Bali tutajaribu kuyapata yote, kadiri tuwezavyo, kwenye kanda.

¹² Sasa, hizi kanda, kila usiku, vitabu na kadhalika, hao wavulana watakuwa navyo nje tu ya jengo pale.

¹³ Sasa, huenda nisiweze kila usiku, kwa kuwa tumejitolea kujaribu kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ku—kuleta hizi Jumbe saba za kanisa, ama Nyakati Saba za Kanisa, katika usiku saba; tukichukua kila usiku, wakati mmoja. Kama vile, Jumatatu usiku, Efeso; Jumanne usiku, Smirna; Jumatano usiku, Pergamo; Alhamisi usiku, Thiatira; Ijumaa usiku, Sardi; na Jumamosi usiku, Filadelfia; na Jumapili asubuhi na Jumapili usiku, Laodikia, wakati wa kanisa tunaishi. Tukionyesha kihistoria kanisa la mwanzoni, na—na wale waandishi na wanahistoria, na malaika wa wakati huo, na—na jumbe, na mwendeleo wa kanisa, jinsi lilivyoshuka hata kufikia wakati huu.

¹⁴ Basi ni la kushangaza sana kuona jinsi kila ubashiri wa Andiko hilo unavyolingana kabisa na historia, kikamilifu

kabisa, kwenye wazo lake. Hata lilinishangaza sana, mpaka, jana, nilikuwa nimesoma hata nikajisikia kana kwamba macho yangu yalikuwa yanavimba. Ndipo nikatoka na kumwambia mke wangu, “Sijawahi kuota hilo kuwa jinsi hiyo.” Mnaona? Jinsi lilivyokuwa ni la ajabu!

15 Na sasa, wakati mwingine, huenda nisiweze kuyamaliza yote katika usiku mmoja, kanisa, ujumbe kwa kanisa. Basi endapo siwezi kuyamaliza, usiku, basi kesho yake asubuhi saa nne. Itatangazwa kila usiku, kwa wale wanaotaka kuja na kusikiliza hayo mengine, maana tunaenda, tutajaribu, kuuweka kwenye kanda. Nitakuwa na ibada basi kuanzia saa mne, asubuhi, niendeleo hadi aduhuri, mchana, kujaribu kuamaliza, ujumbe uliosalia, maana wanaweza kuupata kwenye kanda. Sio . . .

16 Tumetangaza kwamba hakutakuwako na ibada zozote za uponyaji, kwa sababu tunajaribu kuyaweka chini ya matamshi ya kinabii ya Biblia. Halafu, tulikuwa na ibada ya uponyaji hivi majuzi tu hapa. Ndipo baada ya ibada hizi kumalizika, basi tutakuwa na ibada za uponyaji tena mahali hapa.

17 Lakini sasa na—nataka kufanya jambo hili dhahiri kabisa, kusudi kila mtu aweze kukumbuka, ya kwamba sasa, humu ndani, huenda likakata na kuvuta, na kutupa sote mtetemeko mkuu. Lakini ninawajibika, sio kwa—kwa lolote ila kulihubiri Neno. Hilo, ni hilo tu. Ku—kulishikilia tu Neno moja kwa moja. Na mara nyingi huenda, katika nyakati hizi za kanisa, huenda likaakisi juu ya dhehebu la mtu fulani. Basi kama likifanya hivyo, halikusudiwi kuwa ni kwa ukali. Ni—ni kusema tu yale Maandiko yamesema, na ufunuo nilio nao juu Yake. Na ikiwa unafikiri nimekosea, basi usinilaumie hilo, niombe tu kwamba Mungu atanionyesha yaliyo kweli, kwa kuwa hakika ninataka kuwa mkweli.

18 Halafu jambo lingine, nikitambua ya kwamba jukumu nililo nalo, katika—katika mkutano kama huu, kwamba kuwafunza watu, kwamba Roho Mtakatifu ataniwajibisha kwa ajili ya maneno ninayo sema hapa mimbarani. Kwa hiyo mnaona jinsi tunavyoliharibia hili kwa uchaji. Sasa, ninii yetu . . .

19 Ningalikuwa na haya mahali pengine. Lakini, kwa kuwa haya ni mafundisho, basi katika ninii yetu . . . Huko nje kwenye ibada za kiinjalisti, kila mmoja wetu ana wazo ama—ama utambuzi, ama kama vile imekuwa kote katika wakati, nasi tuna makanisa yetu wenyewe, na yale makanisa yetu yaliyotufundisha, na yale tunayoamini. Sisi . . . Sipendi kwenda kwenye kanisa la mtu mwingine, ama miongoni mwa watu namna hiyo, na kusema jambo lililo kinyume na yale watu wamefundishwa. Kwa kuwa, hata hivyo, nimejaribu kutoa matamshi yangu kwamba ninii . . .

20 Ikiwa mtu ni Mkatoliki, naye analitegemea Kanisa Katoliki kwa ajili ya wokovu, amepotea. Ikiwa yeye ni Mbaptisti,

akilitegemea Kanisa la Kibaptisti, amepotea. Ama Mpentekoste, akilitegemea Kanisa la Kipentekoste kumwoko, amepotea. Lakini... Kanisa lolote! Lakini kama mtu huyo binafsi anategemea kwa uchaji imani katika kazi iliyokamilika ya Kristo pale Kalvari, yeye ameokoka, sijali yeye ni wa kanisa gani. Kwa sababu, “Mnaokolewa kwa imani, na hiyo ni kwa neema.”

²¹ Sasa, wakati mwingine, katika kufanya jambo hili, ndipo nitawazia, katika maskini jengo langu dogo hapa tulilolianza miaka mingi iliyopita, kwa maskini bloku za siku nyingi za zege na kadhalika, nalo kwa namna fulani ni mahali patakatifu kwetu. Tunachukua, tunachukua tu kuliona limebadilishwa, kwa njia moja, kwa sababu hapa ndipo Mungu alipoanza kukutana nasi kwanza, wakati hata hatukuwa tumepasakafia. Lakini li—limefikia mahali sasa ambapo linazeeka, nasi tuko katika mradi wa ujenzi—ujenzi hapa, kujaza sehemu hii na kanisa hapa.

²² Sasa, mpaka wakati huo, ninajisikia kwamba wakati nitakaporudi kutoka hudumani, ambapo sitawaudhi ndugu na, ama, jumbe na kadhalika, basi inanipa haki ya kuelezea maoni yangu mwenyewe, ku—kutoka kwa ninii yangu... kutoka mimbarani hapa. Na kwa hiyo kama ukisema, “Nimefunzwa tofauti kidogo,” ningeninii... Halafu basi, katika jambo hili, tunamwalika tu mtu yeyote anayetaka kuja. Mnaona? Hakuna mtu anayeudhamini, ama chochote kile. Ni maskani hapa. Basi mtu yeyote anayetaka kuja, amekaribishwa tu kuja. Njoo tu moja kwa moja. Kwa hiyo ninawaalika mlete Biblia zenu, kila mkutano, na mje na penseli na karatasi.

²³ Na sasa, pamoja na mafafanuzi yote na kadhalika, nisingaliweza kuvileta vitabu hivyo vyote. Kwa hiyo niliandika tu, nikaandika chini, kila wakati, kwenye karatasi hapa, muhtasari kidogo kutoka kwenye historia na mafafanuzi, na kadhalika, nipate kuyasoma tu kutoka kwenye—kwenye muhtasari huu hapa, badala ya kuwa na kitabu na kufungua kurasa. Hata hivyo, inapofikia kwenye Maandiko, tutaitumia Biblia. Halafu basi kwenye mafafanuzi, nitaelezea; ama historia, kwamba ni mwanahistoria yupi aliyesema hilo, na kadhalika. Halafu katika ninii... Hakika, kwa minajili ya kitabu kijacho, mbona, basi tunaweza kulifananisha vizuri basi, na tunaweza kufanya kila kitu vyema.

²⁴ Sasa, tutafanya kila tuwezalo kuanza mapema na kuondoka mapema iwezekanavyo. Itachukua siku nane, mikutano, Jumapili hadi Jumapili.

²⁵ Asubuhi ya leo ninaanza mlango wa kwanza wa Ufunuo, wa Kitabu cha Ufunuo. Nacho Ufunuo kimewekwa katika sehemu tatu. Na milango mitatu ya kwanza ndiyo tutakayokuwa tukishughulikia katika siku nane hizi. Ambapo, wakati mmoja wa kanisa ungetuchukua mwezi mzima. Lakini itatubidi tu

kugusia sehemu za juu, kama tusemavyo. Ndipo mtakapokipata kitabu hicho, kitaandikwa chote, zaidi sana katika utondoti.

²⁶ Sasa, Ufunuo, milango mitatu ya kwanza, inahusu Kanisa, kisha Kanisa linatoweka. Hatulioni tena mpaka wakati wa mwisho. Kuanzia Ufunuo 1 hadi 3, ni Kanisa; Ufunuo 4 hadi 19, ni Israeli, taifa; na 19 hadi 22, ni wote wawili, pamoja. Na yale mapigo na maonyo, na kadhalika, mwishoni! Kimewekwa katika sehemu tatu. Mnaona? Nasi tunachukua milango mitatu ya kwanza, inayohusu Kanisa, na wakati wa kanisa tunaishi.

²⁷ Sasa, kwanza, huenda kidogo ikaonekana kuwa kavu kwa kuwa inatulazimu kurejea nyuma na kuweka msingi. Niliomba na kusoma, na kufanya yote niliyoweza, kujaribu ku—kupata hisi za Roho Mtakatifu, jinsi ya kuliweka hili, watu wapate kuliona, na kwamba muweze, katika kuliona, mpate mwangaza na kuwafanya mumkaribie Kristo, kwa kuwa tuko katika wakati wa mwisho.

²⁸ Na ni jambo la ajabu sana, kwa kuwa nimekuwa nikizisoma historia, nijue jinsi lile kanisa lilivyoanza, na jinsi lilivyoondoka, na kile kilichotukia, na kuona Uzao huo mdogo wa Mungu ukipitia katika kila moja ya nyakati hizo; unakwisha kabisa, karibu unakwisha, katika mahali pamoja.

²⁹ Sasa, kesho usiku, tutaanza, na kuwa na—kuwa na cha—chati hapa; si chati, bali ni ubao wa kuandikia, ambapo kwa namna fulani nataka kulifundishia kwenye ubao. Ninaamini mwalimu wa shule ya Jumapili, mmoja wao, ana ubao. Ninauona huko nyuma. Nitamwomba bawabu aulete huku, auweke hapa mbele, kusudi niweze kufundisha kutoka kwenye ubao huo, na kuyaandika mpate kuwa na uhakika. Nanyi mnaweza kuyachora kwenye karatasi yenu, na kadhalika, na kuliweka vizuri tuwezavyo kulileta.

³⁰ Lakini ninataka kusema tu jambo hili kabla hatujaanza: Kuona mwanzo wa wakati wa kanisa, na kuona jinsi mitume, yale mafundisho, na mambo waliyofundisha, na kanuni za Biblia; na halafu kuliona kanisa hilo, yapata safu ya pili ya mitume, jinsi yalivyoanza kufifia, yale mafundisho halisi, ya kweli; safu ya tatu, yakienda mbali sana; kufikia safu ya nne, lilikuwa limetoweka likawa vu—vuguvugu, hilo kanisa likazaa kanisa vuguvugu.

³¹ Halafu Kanisa lililojazwa na Roho! Ambalo, ninasema hili kwa heshima ya kiungu kwa dini ya kila mtu. Tangu mwanzo, hata wakati huu, Kanisa halisi, la kweli limekuwa ni Kanisa la kipentekoste. Ni kweli. Mungu amelihifadhi Kanisa hili.

³² Nami sikuzote nimeshangaa, wakati Yesu alipotoa lile tamshi, kasema, “Msiogope, enyi kundi dogo, kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ufalme.” Mara nyingi nimeshangaa hiyo inamaanisha nini, bali ninaelewa sasa.

33 Juma lililopita tulikuwa na mkutano huko Shreveport, Louisiana, mkutano mkubwa sana wa kiroho niliowahi kuhudhuria, maishani mwangu. Shreveport!

34 Nilikuwa... Nilikuwa na siku chache za likizo, nami nikashuka kwenda Kentucky pamoja na Ndugu Wood hapa, mmoja wa mashemasi wa kanisa, ama wadhamini, hasa, kuwinda. Tukaingia mwituni.

35 Nilikuwa nimempiga risasi kuchakulo wa kwanza. Nami nikasema, "Nitangoja tu," kwa sababu mtu fulani alipita pamoja na mbwa. Nami nikasema, "Nitangoja tu mpaka kuchakulo warudi kutoka kwenye mashimo. Walikimbia mitini, mashimoni, na kujificha sasa." Nikasema, "Watakapotoka... Nitaketi hapa na kungoja." Kwa sababu, ni baridi sana na kuna ukungu, na masikio yanauma sana. Na, mwajua, u—upepo mkali unapitia kwenye uwazi. Nikasema, "Nitangoja tu mpaka kuchakulo watakapotokea tena."

36 Mara nilipoketi chini, Roho Mtakatifu akasema, "Simama, uende mahali unapopaita 'bonde la mchezaji.' Hapo nitasema nawe."

37 Ndipo nikaenda mahali hapa nilipopaita "bonde la mchezaji." Kwa sababu, kusudi la kulipa jina bonde hilo, mimi mwenyewe, ni kusudi nijue mahali nilipokuwa. "Bonde la mchezaji," ilikuwa ni kwa sababu walikuwa... Niliingia mle na kuona kuchakulo kumi na sita wameketi kwenye mti mmoja; nikapiga risasi kile kiasi kilichoruhusiwa, nikawaacha hao wengine pale, nikaenda zangu. Na huo ndio mchezo, jambo la kufanya. Kwa hiyo basi ninapaita, "bonde la mchezaji."

38 Naye akanirejesha, "Mahali unapopaita 'bonde la mchezaji.'" Si kwamba Yeye alipaita, bali mimi nilipaita hivyo.

39 Ndipo nikapanda juu ya bonde hilo na kuketi chini ya mwaloni mweupe, na kungoja kwa yapata nusu saa, wala hakuna kilichotukia. Nikajilaza chini, nikalala chini kifudufudi, nikainyosha mikono yangu. Ndipo akasema nami.

40 Ndipo alipofanya hivyo, Maneno aliyonifunulia, kwenye Maandiko yaya haya tunayoyaendea asubuhi ya leo, kamwe sikuwa nimeliona hapo kabla, maishani mwangu mwote.

41 Ndipo basi nilipofika Shreveport, Louisiana; mwanamke ambaye ni mwanamke mwenye karama, jina lake ni Bibi Schrader...

42 Miaka mingi iliyopita, wakati Malaika wa Bwana alipokutana nami hapa chini mtoni, mara ya kwanza, na kuonekana katika ile Nuru, na Maneno aliyonena pale; miaka kumi na moja baadaye, wakati nilipoingia kwenye mkutano, maskini mwanamke huyu alisimama na kunena katika lugha na kufasiri. Ilikuwa ni neno kwa neno jambo lile lile yule Malaika alilosema.

43 Na maskini mwanamke yuyu huyu, wakati nilipoingia maskanini kwenye...ama mahali pale huko Shreveport tulipokuwa, Maskani ya Uzima, Roho Mtakatifu alimshukia mwanamke huyo na kusema neno kwa neno yale aliyoniambia huko juu kilimani. Ndipo Roho akaanza kutenda kazi na kutoa tafsiri, akitabiri mambo kwa unafu, kwa unabii, mambo ambayo yangetukia mkutanoni kesho yake usiku, wala halikukosea hata wakati mmoja.

44 Kabla ya hapo, maskini mwanamke mmoja alisimama mkutanoni, mwanamke wa Kibaptisti alikuja kule bila kujua yale angeweza kufanya. Naye alikuwa amesimama katikati ya mkutano ndipo Roho Mtakatifu akamshukia, akaanza kunena kwa lugha, mwanamke Mbaptisti kutoka kwenye Kanisa la Kwanza la Kibaptisti huko Shreveport. Halafu yeye hakujua yale aliyokuwa amefanya. Na kisha, kabla hajasema lolote, Roho Mtakatifu akatoa tafsiri yake, kasema, “BWANA ASEMA HIVI, ‘Katika miezi mitatu, kutakuwako na Roho ya Musa, Eliya, na Kristo, ikihudumu kwenye maskani hii.’” Hapo likatukia, kikamilifu.

45 Mbaptisti mmoja kutoka Meridian, Mississippi, alianza kuweka mkono wake juu ya friji yake, kutoa kitu kwenye friji, ndipo Roho wa Mungu akamjia. Naye akanena kwa lugha, bila kujua alichokuwa akifanya. Na kabla hajapata...hajaelewa alichokuwa akifanya, Roho Mtakatifu akajibu na kusema, “Nenda Shreveport, Louisiana. Mtumishi Wangu atakwambia la kufanya.”

46 Ndipo akaja kule, kasema, “Sielewi hili; halijawahi kutukia hapo kabla.” Loo, jamani!

Tunaishi katika siku za mwisho kabla tu ya kule Kuja kwa Bwana.

47 Kanisa hilo dogo daima limekuwa katika uchache, la Kipentekoste. Simaanishi Wapentekoste wa kimadhehebu. Simaanishi hilo. Bali, watu walio na ujuzi wa kipentekoste! Pentekoste si dhehebu. Pentekoste ni tukio linalomwendea yeyote atakaye. Mkatoliki, Myahudi, Mwongofu, Wamethodisti, Wabaptisti, “Yeyote atakaye, na aje.” Ni tukio ambalo mtu binafsi...Mungu hashughulikii dhehebu, wala hawashughulikii Mataifa kama ja—jamii ama watu. Yeye huwashughulikii watu binafsi, “Yeyote atakaye.” Awe mzungu, mtu mweusi, manjano, hudhurungi; Mmethodisti, Mbaptisti, Mprotestanti, Mkatoliki, chochote alichu, “Na aje,” yeyote yule. Nina furaha sana Yeye alilifanya hivyo. Mimi... .

48 Kama vile yule jamaa alivyosema wakati mmoja, “Ni afadhali nimsikie akisema hivyo kuliko kuliita jina langu, ‘William Branham na aje,’ maana huenda kukawa na William Branham zaidi ya mmoja. Bali aliposema, ‘Yeyote,’ *ninajua* hilo lilinijumuisha mimi.”

Kwa hiyo hivyo ndivyo sisi sote tuanavyoweza kujisikia, “Atakaye, na aje.”

49 Sasa, ninajua kuna watu wengi wanaongojea hapa nje kwenye hoteli na moteli, waliotoka kote ulimwenguni. Mnaona? Wapo watu hapa kutoka Ayalandi na mahali mbalimbali, wanaongojea miadi hii. Lakini siwezi kuishughulikia sasa hivi. Ninataka kuutoa wakati wangu kwa ajili ya hili, mnaelewa.

50 Nitakaporudi kutoka kwenye ziara hizi, kwa kawaida nitarudi ku—kumpata mtu wa kumhudumia, kwa sababu wanaweka miadi. Lakini sasa hivi inatubidi kuwaachilia waende kwa sababu ya Hili.

51 Sasa, jambo moja tu kabla hatujaanza juu ya Kitabu hiki. Hapo mwanzo lilikuwa ni Kanisa la Kipentekoste. Kanisa hilo la Kipentekoste lilitenda kazi kwa nguvu za Roho na kuandika Kitabu cha Matendo. Kwenye safu ya pili, likaanza kufifia, kanisa likawa la kawaida. Wakati wa pili wa kanisa, lilikuwa ni la kawaida sana, lakini ile Mbegu ndogo ya Pentekoste iliendelea kusonga mbele, ile ya kiroho. Kisha ikaingia mahali pa nyakati za giza, za karibu miaka elfu moja mia nne na kitu, za mateso makali. Maskini wakati huo wa Kipentekoste ukaendelea kuishi kupitia hayo. Jinsi ambavyo uliponea hayo, usiniulize. Ilikuwa ni mkono wa Mungu, kitu pekee ambacho kingaliweza kufanya hivyo.

52 Kwa sababu, waliwafunga, kwenye nguzo. Na kuwachukua wanaume na kuwaweka juu ya ki—kisiki, na kuchukua vingi vya mbao na kuichoma miguu yao, na kuwaachilia wanyama, mbwa, wawale kutoka nyuma, wakayavuta matumbo yao, kabla hata hawajafa. Wakawachukua wanawake, wakayakata matiti yao, kwa mkasi namna *hiyo*, matiti yao ya kuume, na kusimama na kuacha damu imwagike, mpaka uhai wao uwatoke. Wakawachukua watoto kutoka kwa mama wajawazito na kuwatupia mbwa na nguruwe, wakati wakiwaangalia. Ukidhaniwa ni Ukristo; bali Biblia ilisema, na Yesu alisema, “Itakuwa kwamba watawaua, wakidhani wanamtumikia Mungu.” Mnaona?

53 Na sasa kitu hicho kilinyemelea mpaka kwenye wakati mwingine. Ndipo hatimaye kikatokea. Ndipo tunaona wakati kanisa likifikia kwenye yale matengenezo, limeondoka na kuondoka, tangu wakati huo, na kumwacha Roho, likamwacha Roho, moja kwa moja hata kufikia wakati huu wa mwisho wakati liko tayari kujiimarisha na kufanya sanamu ya mnyama.

54 Lakini maskini hiyo Roho ndogo itaishi mioyoni mwa watu mpaka Yesu atakapokuja. Haina budi kuishi. Kumbukeni hilo.

55 Tatalichora kwenye ramani, tuchukue historia na kila kitu, na kuwaonyesha ya kwamba ni hivyo hasa. Nikuache uichukue historia, wewe mwenyewe, na kuisoma. Uone kile

Biblia ilichosema, halafu kile historia ilichosema. Uone jinsi zinavyoumana kikamilifu namna hiyo. Loo!

56 Naomba sote tusichukue hili tu kama mhadhara, bali kwa uchaji, kwa uchaji tuchukue maonyo ya Roho Mtakatifu na kuomba, usiku na mchana. Usiache chochote kikuzuie kuomba.

57 Tukiliingilia, litayachimbua maisha ya watu hawa mashuhuri kule nyuma, jinsi walivyojitolea. Utaona jinsi umefanya machache sana. Inanifanya nijionee aibu wakati mwingine, jinsi ambavyo hatuna budi kupata kila kitu kwa urahisi sana, nao walipata kila kitu kwa shida sana. “Walizunguka-zunguka,” Paulo alisema katika Waebrania 11, “wamevaa ngozi za kondoo na za mbuzi, wakateswa na kusumbuliwa, ukiwa.” Ushuhuda wetu utasimamaje karibu na wao? Utasimamaje karibu na huo? Nasi inatubidi kuwa na kila kitu vema sana.

58 Sasa, kwa heshima tu, kabla hatujakifungua Kitabu, ningetaka sisi sote, tunaoweza, kusimama tu kwa dakika moja kwa ajili ya maombi. Sasa kwa uaminifu wa moyo wako, omba dua kwa ajili ya . . . kwa Mungu.

59 Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, na Mpaji wa vipawa vyote vyema na vikamilifu. Tungekuomba, Wewe Bwana, kwanza, kutusamehe kutokujali kwetu kwote, na dhambi zetu na makosa yetu dhidi Yako Wewe, na ya mmoja kwa mwingine na ya wanadamu wenzetu.

60 Jalia wakati huu mdogo wa kuja pamoja usiwe tu kwa ajili ya kuzijenga nafsi zetu wenyewe, bali jalia uwe ni wa kutuangazia sana, na kutuvuvia, hata tutaenda tukawaambie wengine. Jalia uwe ni wakati wa kujiweka wakfu tena, kutuunganisha na Mwili wote wa Kristo na kujiandaa kwa ajili ya Unyakuo.

61 Baba Mungu, si kwa hisia zangu mwenyewe, nikijua ya kwamba mtumishi Wako, na watumishi wengine wote, hawatoshelezi kwa ajili ya kazi hii kuu. Tukitambua jinsi watu mashuhuri, waliotuacha, wameyakinia mioyoni mwao kujaribu kulifunua Hili, ama kuzungumza juu ya Ufunuo huu mkuu; ndipo tunatambua kwamba sisi, zaidi ya walivyo wao, hututoshelezi. Lakini Wewe ndiye utoshelevu wetu.

62 Nami ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utafanya jambo fulani maalum wakati huu, kwamba Roho Mtakatifu atakuwa na mamlaka katika kila moyo. Itahiri midomo inayozungumza na masikio yanayosikia. Na wakati haya yote yatakapokwisha, na tuiweke wakfu Kwako, jalia tutembe kutoka chini ya kizingiti cha nyumba hii, tukisema, “Ilikuwa ni vema kwetu kuwa hapo. Roho Mtakatifu alinena nasi wakati tulipokuwa tumeketi pale. Na sasa tumedhamiria kufanya yote tuwezayo wakati Nuru za jioni zikiangaza.” Tujalie, Bwana.

63 Naomba, wakati wa mkutano huu, uwafanye wanaume na wanawake watie nanga, upya. Naomba uwainue wanenaji kwa lugha, wafasiri wa lugha. Naomba uinue karama za unabii. Wainue wahubiri, wachungaji, wainjilisti, kadhalika, Kanisa lipate kujengwa. Wainue wamishenari waingie hudumani huko ng'ambo na kuileta Injili hii tukufu. Popote Neno litakapoenda, jalia lianguke kwenye udongo mzuri, likizaa mia moja, kwa sababu tunaamini tuko kwenye mwisho wa wakati. Utimilifu umekaribia.

64 Yajalie mambo haya, Baba. Na juu ya yote, Bwana, kwenye wakati huu, unisaidie mimi, niliye mhitaji. Kwa maana naomba hilo, ninapojikabidhi Kwako kwa ajili ya ibada hizi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

[Dada mmoja ananena katika lugha nyingine. Ndugu mmoja anatoa ufasiri—Mh.]

65 Mungu mwenye nguvu, Yule aliyemfufua Yesu katika wafu, tuna furaha sana kujua ya kwamba Roho Wako anaishi miongoni mwetu. Daima Yeye ni mkweli wala hana neno lisilo kweli. Na sasa, Baba, lithibitishe Neno Lako zaidi tunaposoma, kwa ajili ya utukufu Wako. Pia jalia kila moyo, kama ulivyosema, "Uandaliwe na uwe tayari, kwa kuwa kutatokea jambo fulani." Huenda ikawa watu watapokea onyo lao la mwisho kuachana na mambo ambayo wanafanya sasa, waingie kwenye njia ya haki. Tunakushukuru Wewe, Mungu Mtakatifu, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Amina.

66 Tukigeukia sasa Kitabu cha Ufunuo, mlango wa kwanza. Sasa, kwanza, ninataka kusoma vifungu vitatu vya kwanza vya Ufunuo.

Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu, amwonyeshe mtumishi wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana:

Aliyelishuhudia Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, kwa yote . . . mambo yote aliyoyaona.

Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo: kwa maana wakati u karibu.

67 Kama nilivyosema awali, sasa, katika jambo hili tutajaribu kutoa ufafanuzi mdogo sasa wa hiki Kitabu, kulingana na historia na kadhalika. Na kila wakati mnaponiona nikirejea kwenye kurasa nilizoandika hapa, ni mambo ambayo nimetoa kwenye vitabu vya mafafanuzi na kadhalika.

68 Sasa, mwandishi wa Kitabu hiki ni Yohana, mtauwa Yohana Mtakatifu, alikiandikia kizazi cha siku za usoni (A). (B) Kikielekezwa kwa malaika saba wa vipindi saba tofauti vya wakati wa Ukristo, kipindi cha kutoka kwenye siku za mitume

hata Kuja kwa Bwana. Na ninii . . . sasa, nyakati hizi zinafuatana moja kwa moja, kila mmoja, tangu kupaa kwa Bwana wetu hata Kuja Kwake tena. Kila wakati wa kanisa unapewa sifa za hali yake ya kiroho. (E) Kila wakati wa kanisa unaweza kujiangalia kwa Maandiko yake yanayouzungumzia kiroho. Wakati Roho akinena, kila wakati unaweza kujiangalia wenyewe. Kila wakati ulizaa Mzabibu wa kweli wa Kristo, yule Mwanamwali mwenye hekima. Na kila wakati ulizaa mzabibu uliopandikizwa, yule mwanamwali mpumbavu.

⁶⁹ Wanahistoria wanakubaliana, haya ni maisha ya Yohana. Yohana aliishi miaka yake ya mwisho katika mji wa Efeso na akafia mle. Alikuwa kwenye kisiwa cha Patimo, wakati alipokiandika Kitabu hiki, Ufunuo. Haikuwa ni hadithi ya maisha yake, bali hadithi ya Kristo katika nyakati za usoni. Mnaona? Ilikuwa ni unabii. Si maisha ya Yohana, si maisha ya Kristo, bali unabii wa wakati ujao. Haikuwa ni matamshi yake ya kinabii; bali, maonyo ya Bwana, kwa uchaji. Haukuwa ni Ufunuo wa mtauwa Yohana Mtakatifu, bali ni Ufunuo wa Kristo aliye Bwana.

⁷⁰ Ndicho Kitabu cha mwisho cha Agano Jipya, hata hivyo kinaelezea mwanzo na mwisho wa kipindi cha Injili. Wanachuoni wa Biblia wanakubaliana na hayo.

⁷¹ Nyaraka kwa nyakati saba za kanisa ziliandikiwa, kinabii, nyakati za usoni. Paulo aliandika juu ya maisha na utukufu wa yale makanisa saba yaliyokuwako katika siku zake. Yohana aliandika kuhusu maisha na utukufu wa yale makanisa saba katika siku za usoni, ambapo Yohana alikuwa akiwaandikia wachungaji saba ama wajumbe kwa kuwa Wakristo wote wako chini ya malaika hawa saba mbalimbali.

⁷² Sasa, Kitabu cha Ufunuo, sasa tutakichukua, tunapolichambua hili kwa ajili ya asubuhi ya leo na jioni hii. Nasi tutajaribu kuwaachilia yapata saa tano na saa tano u nusu, kitu kama hicho, kisha tuanze tena usiku wa leo kwenye saa moja.

⁷³ Sasa yaliyomo kwenye mlango huu wa kwanza. Kifungu cha kwanza, kwe—kweli kinajieleza Chenyewe, kwa sababu ni Ufunuo wa Yesu Kristo. Kifungu cha pili, mtauwa Yohana Mtakatifu ndiye mwandishi na mtumishi. Kifungu cha tatu, baraka zinatangazwa. Kifungu cha 4 hadi cha 6, salamu kwa kanisa. Kifungu cha 7, matangazo. Kifungu cha 8, Uungu mkuu wa Yesu Kristo. Kifungu cha 9 hadi cha 20, lile ono la Patimo.

⁷⁴ Na, pia, kifungu cha 14 na cha 15 vinaelezea utukufu Wake wenye sehemu saba za Utu Wake. Loo, ni la kupendeza tunapomwona Kristo katika utu Wake wenye sehemu saba za ninii ya-. . . utu Wake wenye sehemu saba, katika ufufuo Wake wenye utukufu.

⁷⁵ Sasa, kichwa chake kinatoa sifa zake.

Ufunuo wa Yesu kristo, . . .

76 Si ufunuo wa mtauwa Yohana Mtakatifu, bali Ufunuo wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

77 Sasa, neno la Kiyunani la *ufunuo* ni *apocalypse*, ambalo linamaanisha “kuonyesha.” Nami nilikuwa nikilichukua neno hilo na kulichunguza. Linamaanisha, *apocalypse*, ni kuninii . . . Kama vile mchonga sanamu, amechonga sanamu kubwa, naye ameifunika kwa pazia. Ndipo basi anaenda na kulipasua na kuliondoa pazia hili na kufunua alichu nacho nyuma ya hilo pazia. Ni kufunua.

78 Nacho Kitabu hiki sio kuufunua, sana sana, Utu wa Yesu Kristo. Hata hivyo, bila shaka kinanena juu ya Uungu Wake na utu Wake wenye sehemu saba, na pia juu ya mambo aliyo Yeye, kama vile Kuhani, Mfalme, na kadhalika. Lakini ni kufunuliwa kazi Zake za usoni katika nyakati Zake saba zijazo za kanisa. Ni . . .

79 Wakati Bwana wetu alipokuwa duniani, wanafunzi walimwuliza, na kusema, “Bwana, wakati huu utairudishia Israeli ufalme?”

80 Naye Yesu akasema, “Si juu yenu kuujua wakati huu wala majira.” Wala hakuna mtu angejua. Kasema, “Hata Mwana,” bado, “hakujuu.”

81 Bali baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, na kupaa Utukufuni, Yeye alipokea kutoka kwa Mungu mambo ya usoni ya Kanisa. Ndipo akarudi, apate kuuleta Ujumbe huu kwa Kanisa, na Ujumbe huu wa kuja Kwake na hali ya makanisa Yake kote katika Wakati.

82 Yeye asingeweza kufanya hivyo kabla ya mauti, kuzikwa, na kufufuka Kwake, kwa kuwa bado hakuwa amejua hayo. Lakini mliona jinsi Maandiko yanavyosema hapa?

Ufunuo wa Yesu Kristo, ambao Mungu alimpa (Kristo), . . .

83 Jinsi ambavyo Mungu Baba alimpa Mwanawe Yesu Kristo Ufunuo. Naye akamtuma malaika Wake kwa Yohana, kuonyesha mambo haya yaliyokuwako; yaliyokuwako, yaliyopo, na yatakayokuwako. Loo, limewekwa vizuri!

84 Sasa, katika wakati huu mkuu ujao ambao Yohana aliuona! Sasa, huu, Ufunuo huu alipewa yeye, pekee, apate kufunua kusudi maalum la Kristo, kile ambacho angekuwa na angeonekana, katika kila wakati. Hiyo ndiyo sababu nilisema, asubuhi ya leo, weka nia yako kwenye Kanisa la kweli. Kanisa la kweli lilianza kwenye Siku ya Pentekoste.

85 Hakuna mwanatheolojia, msomi wa Biblia, ama mwanahistoria, anayeweza kamwe kusema ya kwamba lilianza kwenye siku ya Martin Luther, Wesley, wakati wa Katoliki, wala wakati mwingine wowote. Lilianza pale Pentekoste. Huo

ulikuwa ndio uzinduzi wa Kanisa. Huo ulikuwa ndio mwanzo. Kwa hiyo, basi, katika majadiliano na mtu yeyote, simama kwenye lango hilo la Pentekoste, wala hawawezi kwenda mahali pengine popote.

⁸⁶ Ni kama tu kumweka sungura shambani. Unajua mahali kila shimo lilipo, kwa hiyo umeliziba kabisa. Itambidi kurudi mahali papa hapa alipoingilia.

⁸⁷ Vema, hivyo ndivyo, mtu yeyote anayezungumza juu ya makanisa na nyakati za kanisa, na matendo ya Roho Mtakatifu, itakubidi kurudi kwenye cha asili, mwanzoni. Inabidi irudi kule kwa sababu Mungu hana kikomo, Naye yuna nguvu zote. Kwa hiyo, Yeye akiwa hana kikomo, hawezi kufanya jambo fulani *hapa*, kisha afanye kinyume chake, *huku*. Hana budi kufanya kila wakati jinsi alivyofanya mara ya kwanza.

⁸⁸ Kama vile Petro alivyosema, kwenye siku ya . . . hapo Mataifa walipompokea Roho Mtakatifu, yeye alisema, “Je, tunaweza kukataza maji, kwa kuwa hao wamempokea Roho Mtakatifu jinsi tulivyompokea hapo mwanzo?”

Yesu, wakati alipokuwa duniani, alinena na kusema, “Ni . . .”

⁸⁹ Mtu fulani alikuja na kusema, “Je, ni halali kwetu, kuwatupa nje wake zetu kwa sababu yoyote?”

⁹⁰ Yesu akasema, “Yeye aliyemuumba mwanamume, alimuumba mwanamke. Kwa sababu hii mwanamume ataninii . . .”

Akasema, “Lakini Musa alituruhusu kuandika barua ya talaka.”

Yesu akasema, “Haikuwa hivyo tangu mwanzo.”

⁹¹ Rudini kwenye mwanzo. Kwa hiyo, kama tutazungumza juu ya wakati wa kanisa, inatubidi kurudi kwenye mwanzo, tukiweka kando kila tamshi ambalo mtu yeyote ametoa kote katika wakati.

⁹² Hiki ndicho Kitabu rasmi sana cha Kitabu chochote katika Biblia. Hiki ndicho Kitabu cha pekee ambacho Kristo alitia muhuri Wake juu yake. Kinaanza na baraka na kuishia kwa laana. “Heri yeye asomaye.” Na, “Amelaaniwa yeye anayeondoa lolote Kwake.”

⁹³ Ndicho Kitabu cha pekee ambacho Kristo alikiandika, Mwenyewe, katika Biblia nzima. Zile Amri Kumi, Yeye aliziandika kwa kidole Chake. Hiyo ni kweli. Wayahudi walizishikilia hizo. Na, leo hii, ni—ni Ufunuo.

⁹⁴ Na kama Shetani anachukia Kitabu chochote katika Biblia, ni Ufunuo. Kuna viwili . . . Yeye anayachukia Maandiko yote, na ni vitabu vyote rasmi vya Maandiko. Lakini, kwa jumla, vile anavyochukia zaidi sana, ni Ufunuo na Mwanzo. Kwa

sababu, Mwanzo kinaonyesha ule mwanzo. Ufunuo kinafunua kile kitakachompata katika siku ya mwisho. Yeye atafungwa kwa muda wa miaka elfu moja; kisha yeye, pamoja na nabii wa uongo, na yule mnyama, watatupwa, wangali hai, kwenye Ziwa la Moto.

⁹⁵ Naye atakipinga Kitabu cha Mwanzo kuhusu—kuhusu kuwa ni cha kweli. Atasema, kwamba, “Sio sahihi.” Naye atachochea mawazo ya watu. Angalieni mahali ibilisi anapokaa, hicho Kitabu cha Mwanzo ama Kitabu cha Ufunuo, cha kwanza na cha mwisho.

⁹⁶ Nacho Kitabu cha Ufunuo kina mifano mingi ndani yake kuliko Vitabu vingine vyote katika Biblia. Kina mifano zaidi kwa sababu ni Kitabu cha unabii. Ni Kitabu cha unabii. Kwa hiyo kinapaswa kueleweka na tabaka la kinabii. Kitabu hiki hakikukusudiwa kila mtu. Hakuna mtu anayeweza kukielewa, ni vigumu. Kitabu hiki kimetengenezewa tabaka fulani la watu. Huko katika Kumbukumbu la Torati, kinasema, “Mambo ya siri ni ya—ya—ya Bwana.” Hiyo ni kweli. Naye anatufunulia, watoto Wake, mambo yaliyofichika. Kwa hiyo hakiendi . . .

⁹⁷ Nia ya kimwili haiwezi kufahamu hayo mambo makuu ya Maandiko, kwa sababu ni upumbavu kwao. Bali kwa wale ambao wanalipenda Neno la Mungu, hao ndio walioandikiwa hiki Kitabu, kwa Kanisa. Ufunuo wa Yesu Kristo, “Kwa kanisa lililoko Efeso, kwa kanisa lililoko Smirna, kwa kanisa, kwa makanisa,” na kuendelea. Ufunuo wa Yesu Kristo kwa Kanisa. Ninapenda hilo.

⁹⁸ Basi angalieni, pia ndio ukamilisho wa Maandiko, ukamilisho mkamilifu. Na kimewekwa mahali pake halisi kijiografia, mwishoni mwa Biblia. Ufunuo wa kitu hicho chote umewekwa hapa nyuma pamoja na baraka kwa yeye alisomaye na kulisikia, pamoja na laana kwa hao watakaongoza ama kutoa. Ni kitabu rasmi kikamilifu, loo, ile yakini. Hakuna kitu kinachoweza kuongezewa Kwake. Ndipo mtu anapojaribu kutoa chochote kutoka Kwake, au kuongeza chochote Kwake, Mungu alisema ataondoa sehemu iyo hiyo kutoka kwenye Kitabu cha Uzima. Mnaona? Angeondoa sehemu yake kutoka kwenye Kitabu, ikiwa angeongeza Kwake.

⁹⁹ Kwa hiyo, tunapoona Ufunuo wa namna nyingi wa Bwana wetu, kwamba Yeye ni nani, Yeye ni nini, kama mtu yeyote ataongeza kitu fulani Kwake ama kuondoa kitu chochote Kwake, ni unabii wa uongo. Wengi wamejaribu kusema walikuwa na jambo fulani jipya kuliko Hilo. Lakini Huo ndio Ufunuo mkamilifu wa Bwana Yesu katika wakati Wake wa kanisa na katika Siku Yake, Ufunuo wa Bwana wetu.

¹⁰⁰ Sasa—sasa, *kufunuliwa*, neno la Kiyunani, kitu ambacho kimekuwa kimefichwa, kufunu-. . . “kumfunua” Kristo.

Sasa, kifungu kifuatacho, tunaona, katika kifungu cha pili.

¹⁰¹ Kifungu cha kwanza ni kumfunua Kristo, Ufunuo, ama kufunua. Loo! Jinsi ambavyo wakati wa mwisho na kule Kuja kwa Bwana kuli-. . . kulivyofunikwa, kwa mitume! Waliuliza swali, ila ni mmoja tu aliyeishi apate Ufunuo huo. Na hata hivyo, yeye hakuufahamu, kwa kuwa historia haikuwa imefanywa bado.

¹⁰² Sasa, historia ya Kitabu hiki, ama ya—yaliyomo kwenye Kitabu hiki, yalielekezwa kwenye yale makanisa saba katika Asia Minor, yaliyokuwako wakati huo. Yalielekezwa kwa makanisa hayo saba. Kulikuwako na makanisa mengi kuliko hayo saba, siku hizo. Lakini kila moja ya makanisa hayo lilikuwa ni muhimu kwa tabia ya kanisa hilo, ambayo ingelifuata kote katika wakati, tabia ya kanisa hilo. Kama vile Efeso, ilikuwa na tabia. Smirna, Pergamo, na kuendelea, Filadelfia, kila moja ya makanisa hayo lilikuwa na tabia ndani yake, ambayo ingejitokeza tena katika nyakati zijazo. Loo! Laiti mngaliweza tu. . .

¹⁰³ Kuna mtu yeyote anayeweza kuona ma—matumizi ya kiroho ya Maandiko na aweze kusema kwamba hayakuvuviwa? Tendo lako lenyewe, nia yenyewe, makusudi yenyewe ya watu, mbona, inathibitisha ya kwamba Maandiko yamevuviwa, kuona jinsi ambavyo Mungu anayatumia mambo hayo. Yale tu unayofanya, *hapa*, ni mfano wa kitu fulani.

¹⁰⁴ Kama vile Ibrahimu akimtoa Isaka dhabihu, mwanawe wa pekee; mfano wa Mungu akimtoa Mwanawe, mamia ya miaka baadaye. Jinsi Yusufu alivyouzwa na alivyokuwa gerezani, akachukiwa na ndugu zake na kupendwa na baba yake; Yesu, katika mfano. Jinsi Roho alivyotenda kazi kupitia kwa Yusufu, mtu, na kwa urahisi akafananisha maisha ya Kristo, kikamilifu. Jinsi ambavyo, Daudi, Mwana wa Daudi alivyoketi kwenye mlima ule ule. Wakati Daudi alipokataliwa kama mfalme kisha akapanda kile kilima, Mlima wa Mizeituni, akiangalia nyuma, akilia, kama mfalme aliyekataliwa; miaka mia chache baada ya hapo, Mwana wa Daudi alipanda kilima kile kile, kama Mfalme aliyekataliwa, na kuulilia Yerusalemu. Roho akiwa katika mfano na umbo. Loo!

¹⁰⁵ Basi mnaweza kuliona lile Kanisa kuu la kipentekoste katika siku hizi za mwisho? Mnaweza kuona jinsi Mungu alivyolianzisha kwenye Siku ya Pentekoste? Huyu Roho anapaswa kubaki Kanisani kupitia nyakati zote.

¹⁰⁶ Wakawa wa kawaida na wasiojali. Iliwabidi kuwa na dhehebu. Iliwabidi kuunganisha kanisa na taifa pamoja, na hatimaye wakafanya hivyo na kusababisha mamia ya miaka ya mateso. Halafu, yale Matengenezo, wao wakatoka. Na kila mwaka, wamekuwa wakikatilia mbali kutoka kwenye Roho na kuongezea kwenye mambo ya kawaida, kumwondosha Roho na kuongezea kwenye mambo ya kawaida, mpaka sasa wako tayari

tu kufanya hivyo tena. Tunaishi kwenye majira haya ya mwisho, ya kumalizia, ukamilisho wa kanisa. Tuko katika Filadelfia . . . ama Wakati wa Kanisa la Laodikia.

¹⁰⁷ Sasa, mlango wa kwanza, kifungu cha kwanza, kilitambulishwa kwa—kwa Yohana. Sasa, mwandishi wake ni nani? Yohana. Yohana. Haukuwa ni ufunuo wa Yohana, nasi tunajua ya kwamba haukuwa, kwa sababu ulikuwa ni Ufunuo wa Bwana Yesu Kristo. Yeye alikuwa hivi, alichaguliwa kuwa mwanafunzi. Nacho Kitabu Chenyewe kinafunua kile kitu kilichokuwa, Yesu Kristo, kwa yule Yeye alikuwa akimfunua.

¹⁰⁸ Nao ulitumwa kwa . . . “Naye akautuma kwa Yohana kwa mkono wa malaika wake.” Hatujui huyo malaika alikuwa ni nani. Biblia haisemi huyo malaika alikuwa ni nani. Lakini tunajua ya kwamba alikuwa ni nabii, maana Biblia baadaye ilisema, ya kwamba, “Mimi Yesu nimemtuma malaika wangu kushuhudia mambo haya ambayo hayana budi kutukia upesi.”

¹⁰⁹ Ndipo tunaona ya kwamba wakati Yohana alipoanza kumwabudu huyo malaika, huyo malaika alisema, “Angalia usifanye hivyo.” Ufunuo 22, naamini ndipo. Naye akasema, “Kwa kuwa mimi ni mtumishi mwenzako na wa manabii.” Huenda ilikuwa ni Eliya. Huenda ilikuwa ni mmoja wa hao manabii. Yohana alikuwa ni mtume. Bali nabii huyu alitumwa.

¹¹⁰ Naye Yohana, akiwa ni mtume, hebu angalieni tabia ya hizo injili zake zingine, inathibitisha kwamba Yohana siye aliyekiandika, kwa sababu hakina tabia za Yohana. Hebu chukueni Yohana wa Kwanza, Yohana wa Pili, kadhalika, na mvisome. Kisha mwangalie tabia yavyo, halafu mwangalie tabia ya hiki. Yohana alikuwa ni mwandishi na alikuwa ni mtume, bali hii ni roho ya nabii. Ni mtu tofauti, kwa jumla. Mnaona? Hayakuwa ni maandiko ya Yohana. Haukuwa ni ufunuo wa Yohana. Ulikuwa ni Ufunuo wa Mungu wa Yesu Kristo kwa makanisa. Na ilikuwa . . . Yohana alikuwa ni mwandishi tu, mwandishi, na—nacho hiki Kitabu kinatangaza vivyo hivyo.

¹¹¹ Sasa, hakikuandikiwa Yohana. Kiliandikiwa Kanisa. Vema. Yohana, wakati huo, alikuwa ndiye mchungaji wa kanisa la Efeso. Na sasa Kitabu hicho kimeandikiwa Yohana . . . ama kanisa, sio Yohana.

¹¹² Sasa kifungu cha 3, Yeye anatangaza baraka. Sikilizeni hili.

Heri asomaye na hao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo: kwa maana wakati u karibu.

¹¹³ Ni wakati gani ulio karibu? Wakati mambo haya yatakapotukia, wakati Ufunuo huu wa Yesu Kristo utakapokamilika katika kila wakati wa kanisa.

¹¹⁴ Sasa sababu ya Yeye kukiandika jinsi hii. Kama angalisema, “Vema, sasa, Yeye . . .” Walikuwa wakimtamazia kufanya

hivyo; kama ilikuwa imefunuliwa, kama Yeye . . . ingalifunuliwa kwa Yohana, ya kwamba Yeye atakuja mara makanisa hayo yatakapomalizika. Hivyo ndivyo Yohana alivyoliwazia. Lakini kama ilikuwa hivyo, hayo makanisa, mara yalipomalizika, yaje. . . Kama alijua, kama ilikuwa imefunuliwa kwake kutakuwako nyakati saba ndefu za kanisa, miaka elfu kadhaa, ama miaka mia kadhaa, basi kusingekuwako na sababu ya kungojea. Wangeliishia tu wakati wao wa kanisa.

115 Kwa hiyo, Mungu alilineni, wala halikufunuliwa kwao. Halikufunuliwa Martin Luther, mambo ambayo John Wesley alijua kuhusu Maandiko. Halijafunuliwa Wabaptisti, yale Wapentekoste wanayojua kuhusu Maandiko, kwa sababu ni wakati mwingine. Ni majira mengine. Naye Mungu huyafunua mambo Yake katika majira yake tu. Loo!

116 Huwezi kupanda mahindi kwenye msimu wa kuchipusha na kuvuna wakati uo huo. Unapanda mbegu nayo inakua ikakomaa. Mungu hupanda Neno Lake na halafu linakua moja kwa moja. Ndipo tunaangalia nyuma na kusema, “Hilo hapo.” Mbona, hakika, tunalionika likiisha kufunuliwa.

117 Sasa, “Heri,” Neno, tangazo la baraka, kwenye kifungu cha 3, “kwa hao wasomao ama kusikia siri zake.”

118 Hufanya . . . nia ya kimwili hupuza hili, kwa sababu nia ya kimwili haijui kitu juu yake. Si ajabu nia ya kimwili hailijui, kwa sababu ni Shetani ndani ya hiyo nia ya kimwili. Naye Shetani amefichuliwa, naye Shetani hataki kufichuliwa.

119 Mmeona jinsi lilivyo jambo la kuchukiza kwa Shetani wakati anapofikiri anaenda kufichuliwa? Angalieni kwenye moja ya ibada hizi. Angalieni matendo ya watu. Angalieni, mkutanoni. Kabla tu Shetani hajafunuliwa, juu ya mtu fulani, ungeona uso wao ukibadilika. Unaona, hawajui wawazie nini. Mara, Roho Mtakatifu anashuka na kumfunua ibilisi huyo. Loo! Yeye anauchukia mkutano wa namna hiyo. Hiyo ndiyo sababu tumekuwa na vita jinsi hiyo, kwa sababu Neno la Mungu humfichua ibilisi. Mnaona? Linaeleza kwamba yeye ni nani.

120 Kama vile mnavyosema, “Mwanamke huyu anayeketi hapa,” chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, kasema, “jina lake ni Bibi Jones. Anatoka Ninii.” Hilo linafanya nini? Linaichukua roho yake, linaleta mpaka mahali fulani.

121 “Unanijua? Mtu huyo hanijui mimi, kwa hiyo haina budi kuwa ni roho fulani. Ni roho ya aina gani?”

“Ni Roho wa Mungu.”

“Vipi? Nina shida gani?”

122 “Una kifua kikuu, kansa,” chochote kile, “lakini BWANA ASEMA HIVI. . .”

“Loo!” Loo, jinsi Shetani anavyochukua hilo, kwa maana linamfichua.

¹²³ Sasa, nia ya kimwili inaangalia tu, inasema, “Kusoma akili, telepathia ya akili.” Hawajui. Ni upumbavu kwao.

¹²⁴ Lakini kwa wale wanaojua kwamba Hilo ni nini, loo, ni baraka jinsi gani! Ni kitu gani? Ufunuo. Ufunuo wa nani? Wa mtu aliye mimbarani? Wa Yesu Kristo katika wakati huu wa mwisho wa kanisa, akijifunua Mwenyewe kama alivyoahidi angefanya. Mnaona?

¹²⁵ Ni ufunuo, mnaona, naye Shetani anauchukia huo. Jamani, jinsi anavyouchukia! Yeye amefichuliwa, unaukichua mpango wake. Shetani anauchukia Ufunuo na Mwanzo, nimeliandika hapa. Hiyo ni kweli kabisa.

¹²⁶ Sasa, kwa nini anauchukia ufunuo? Ni kwa nini anauchukia sana ufunuo? Ni kwa sababu vitabu vyote rasmi vya Neno la Mungu na Kanisa la Mungu vimejengwa kwa uchaji juu ya ufunuo.

¹²⁷ Kamwe hautafundishwa shu—shuleni, haijalishi tuna seminari ngapi nzuri. Ziko huko nyuma katika nyakati za giza. Biblia pamoja na Kanisa ni ufunuo mtupu.

¹²⁸ Hebu tufungue, nina Maandiko yaliyoandikwa hapa, Mathayo, m—mlango wa 16 na kifungu cha 18. Hebu tuangalie kidogo—kidogo tu Mathayo 16:18, tuone mahali Maandiko yalipo, ambapo ni ufunuo. Akishuka kutoka mlimani, kifungu cha 17.

Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe, Simoni Bar-yona: kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.

Nami nakuambia. . . wewe, . . . wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.

¹²⁹ Sasa, kanisa Katoliki husema, “Yeye alilijenga juu ya Petro.” Vema, hayo, hayo kweli ni mawazo ya kimwili. Usingeweza kuwazia nia ya kiroho ikilielewa jambo kama hilo; ambapo Mungu, huku Mwanawe Mwenyewe amesimama pale, na hata hivyo alijenge Kanisa Lake juu ya mtu wa kawaida, kabwela, aliyezaliwa katika dhambi. Mtu huyu alilithibitisha. Yeye, roho yuyo huyo akiwa juu yake, alimlaani Yesu na kumkana papo hapo usoni Mwake. Haikuwa ni Petro.

¹³⁰ Ama, wala haikuwa mwa—mwamba uliokuwa umewekwa pale, kama makanisa mengine yanavyodai ilikuwa. Haikuwa ni mwamba. Maana, Petro. . .

¹³¹ Huo mwamba aliokuwa akinena habari zake hapo, haukuwa ni Petro, wala haukuwa ni Yeye.

¹³² Sasa, watu wengi wa Kiprotestanti hujaribu kusema, “Ilikuwa ni Yesu. Yeye alilijenga Kanisa hilo juu ya nafsi Yake. Yeye!” La, hilo lingali si kweli. Kama ukiangalia, haikuwa ni Yesu, wala haikuwa ni Petro. Ilikuwa ni ufunuo.

...mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni amefanya ufunuo huu.

133 Angalieni. Ninataka kuwaulizeni. Katika bustani ya Edeni, hakukuwako na Maandiko yaliyoandikwa. Halafu hao wavulana wawili, Kaini na Habili, nao wote wawili walitaka kutoa sadaka na kupata kibali kwa Mungu. Walipofanya hivyo, Kaini alikuja akajenga madhabahu; Habili akajenga madhabahu. Vema, kama hayo ndiyo tu Mungu anayohitaji, Mungu angekuwa asiye na haki kumhukumu Kaini. Vema. Basi Kaini akatoa sadaka; na Habili pia. Wote wawili walitoa sadaka. Kaini aliabudu, na Habili pia. Kaini alifanya kila kitu alichofanya Habili.

134 Kwa hiyo kama kwenda kanisani, kuwa mfuasi wa kanisa, kutoa sadaka, na kuomba, na kumwabudu Mungu, ndiyo yote Mungu anayohitaji, basi Mungu angekuwa asiye haki kumhukumu Kaini kwa kufanya vile Yeye alisema afanye.

135 Lakini, unaona, Habili, kwa ufunuo, yeye alijua tunda silo lililowatoa kwenye bustani ya Edeni, kama vile watu wengi wa kimwili wanavyodhani siku hizi. Habili alikuja na kutoa tunda la shamba, na Mungu akalikataa, bali ilifunuliwa... Ninamaanisha, Kaini alitoa, samahani. Kaini alitoa tunda la shamba maana alifikiri hilo ndilo lililowatoa kwenye bustani ya Edeni. Angalia ufunuo huo. Angalia ubishi wake. Angalia jinsi unavyoudhi siku hizi. Bali tunda silo lililowatoa humo. Hawa kamwe hakula matofaa yoyote. Hakika. Yeye alitambuaje alikuwa yu uchi, kama alikula tofaa? Iihusu maisha ya kujuana kimwili. Ilibidi iwe hivyo!

136 Sasa, tutachukua hilo kama somo, nasi tumelichukua, tutalirejea. Hawana Andiko hata moja.

137 Baadhi yao wanasema, “Vema, yeye alisema, ‘Nimepata mwana kutoka kwa Bwana.’” Naam, bwana. Vivyo hivyo na kahaba pia. Mungu hana budi kufanya uhai wote.

138 Lakini ni maisha yaliyopotoka. Hebu angalieni tabia ya mvulana huyo. Yeye alikuwa ni wa baba yake, ibilisi; chuki, katili, mwuaji. Mnaona?

139 Halafu basi jinsi, Habili, wakati wao... wazazi wake labda walimwambia ya kwamba—ya kwamba hiyo miti ilikuwa na tunda, na kadhalika. Lakini, ilifunuliwa kwa Habili. Habili alitoka akaenda akamchukua mwana-kondoo, kwa ajili ya damu, kutoa uhai. Sio mti wa matunda, unaoleta matofaa na ndizi na peasi. “Lakini Habili, kwa ufunuo wa kiroho,” Waebrania 11, “alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi. Mungu akiishuhudia, kwa maana ilifunuliwa kwake kwa imani.”

140 Hapo ndipo Mungu alipolijenga Kanisa Lake. “Kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili.” Kamwe hukulisoma katika seminari. Mtu fulani kamwe hakukufundisha Hili mahali fulani. “Ila Baba Yangu aliye mbinguni amekufunulia Hili.”

Hapo, kitu hicho chote ni juu ya ufunuo, Kanisa lote, “Juu ya mwamba huu wa Ufunuo wa Yesu Kristo, nitalijenga kanisa langu.”

¹⁴¹ Huenda ukachukua yale mchungaji asemayo. Huenda ukachukua yale seminari inayofundisha. Huenda ukachukua yale kanisa lisemayo. Wala si kweli, bado. Huenda ukaweza kulielezea kwa ufasaha. Bali mpaka Mungu amekufunulia ya kwamba Yesu Kristo ni Mwanawe, nawe umeokolewa kupitia kwa Damu Yake; juu ya ufunuo huo, kwamba, “Yeye ni Mwokozi wangu.”

¹⁴² “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

¹⁴³ Kwa hiyo basi unaona ni kwa nini Shetani anakichukia sana Kitabu cha Ufunuo. Chochote ambacho kimefunuliwa, ufunuo wa kiroho, Shetani anakichukia. Hiyo ndiyo sababu anaipinga sana huduma hii siku hizi. Kwa sababu, ni kitu gani? Kufunuliwa kwa Kristo.

¹⁴⁴ Acha kanisa liendeleo na madhehebu yake makuu na mashirika, na maskini jumbe zake zilizopambwa vizuri na kadhalika. Acha waendeleo, Shetani hatalisumbua hilo. Hawana shida. Kila mtu anawapigapiga mgongoni.

¹⁴⁵ Wakati unapofika ambapo Mungu, kwa Roho Mtakatifu, anamfunua Kristo tena Kanisani, kwa nguvu na madhihirisho ya kuwaponya wagonjwa, na kufanya ishara ambazo Yeye alisema zingewafuata waaminio, zitimie, basi Shetani anapinduka kitandani mwake. Anafanya jambo fulani kulihusu. Mpaka wakati huo, Shetani hajali unajiunga na kanisa kiasi gani. Hajali ni kiasi gani. Bali wakati Kristo anapokufunulia ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, na kazi alizofanya wewe unazifanya pia; sio kazi zingine, bali kazi zile zile.

¹⁴⁶ “Yeye aniaminiye mimi. . .” Yohana Mtakatifu 14:7. “Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Atafanya kazi zile zile, na kubwa kuliko hizi.” Kwa sababu, Kristo asingeweza kuhubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu, ungekuwa ni mkubwa zaidi. Asingeweza kuwaletea, kwa sababu Roho Mtakatifu hakuwa ametolewa bado. Lakini wakati Yesu alipokuja na kuutoa Uhai Wake sadaka, naye Roho Mtakatifu akarudi, basi wangeweza kuwapa watu Uzima wa Milele. Hizo ndizo “kubwa zaidi.”

¹⁴⁷ Lakini ishara na maajabu, Yesu alisema dhahiri, katika Marko 16, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe.” Umbali gani? Ulimwenguni kote. Wangapi? Kila kiumbe. Maadamu Injili inahubiriwa, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Na wakati hilo linapokuwa ni ufunuo, ndugu, umeukaribia ule Ufalme basi. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

148 Kwa sababu, mwanamume ama mwanamke aliyewahi kuwa kwenye lile jangwa huko nyuma peke yake, kama Musa alivyokuwa, na ufunuo wa Mungu umedhihirishwa kwake kupitia kwa Roho Mtakatifu, hakuna kitu kinachoweza kumtikisa. Yeye ni mzima na imara tu awezavyo kuwa.

Shetani anachukia Ufunuo. Haupendi, hata kidogo; unaivuruga mipango yake.

149 Tabia ya Kitabu hiki inaonyesha ya kwamba Yohana hakukiandika. Hiyo ni kweli. Kwa kuwa ni—ni kwa ajili ya wengine. . . Haya ni maandishi yake, bali sio uvuvio wake. Ni uvuvio wa Mungu ndio unaokiandika Kitabu hiki. Vema.

150 Hebu tuone vile kinavyosema sasa.

Heri asomaye na wao wayasikiao. . . unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo: kwa maana wakati u karibu.

151 Sasa, “Wakati umekaribia.” Kitu gani? Wakati Ufunuo kamili wa Yesu Kristo umefanywa ujulikane kwa makanisa Yake. Na huku nyakati zote zikipita, unafunuliwa tu kwao.

152 Sasa tuko moja kwa moja kwenye wakati wa mwisho, kwa hiyo sasa kweli tuko kwenye mwisho wa ulimwengu. Tuko katika ukamilifu wa historia ya ulimwengu. Na kabla juma hili halijaisha, na Mungu akiwa yu pamoja nasi, akitusaidia, tutathibitisha ya kwamba tuko kwenye ukamilifu wa nyakati za kanisa. Tuko katika Filadel- . . . ama Wakati wa Kanisa la Laodikia, ukamilifu wa nyakati zote. Tuko kwenye ukamilifu wa ulimwengu wa kisiasa. Tuko kwenye ukamilifu wa—wa ulimwengu wa kawaida. Tuko kwenye ukamilifu wa vitu vyote. Tuko katika mwisho wa kila kitu cha kawaida, tukiwa tayari kuingia.

153 Nilipokuwa nikija hivi majuzi, ninaamini nilikuwa nikienda Shreveport, ama kuja mahali fulani. Nikaangalia. Nikasema, “Miti inakufa. Nyasi zinakufa. Maua yanakufa. Ninakufa. Ulimwengu unakufa. Kila kitu kinakufa.” Tumekeki hapa asubuhi ya leo, tukifa.

154 Hakika kuna ulimwengu mahali fulani, ambapo kila kitu hakifi. Endapo kuna mmoja ambapo kila kitu kinakufa, hapana budi kuwe na mmoja ambapo kila kitu kinaishi. Huo ndio tunaotamani, kufika mahali hapo ambapo pana. . . miti inasimama isiyopatikana na mauti. Loo, ambapo kila kitu hakipatikani na mauti na kinasimama katika—katika utukufu wa Mungu.

155 Sasa, sasa, vifungu vitatu vya kwanza ambavyo tumekuwa navyo sasa, tukiweka msingi. Cha kwanza, “Ufunuo wa Yesu Kristo.” Cha pili, “Ulitolewa kwa Yohana kwa mkono wa malaika.” Na cha tatu, ni, “Heri, heri kwa hao wasomao,

na,” endapo huwezi kusoma, “heri yeye asikiaye.” Huwezi kusoma? Wewe lisikie tu. Hivyo tu. “Heri yeye asomaye, na,” endapo huwezi kusoma, “heri yeye asikiaye, kwa kuwa wakati umekaribia.”

¹⁵⁶ Sasa, wazia kile kitabu rasmi cha huu kinachomaanisha, ni kwamba, Yohana, yule mwandishi hapo, katika kuuandika, alikuwa... *Huyu* ni Yohana hapa, akisema tu “heri” na kadhalika. Sasa, kile ninachowazia ilikuwa, katika Agano la Kale, kuhani alisimama asubuhi na kusoma Maandiko. Kusanyiko likasikiliza. Wengi wasingeweza kusoma. Kwa hiyo akasema, “Heri yeye asomaye, na yeye asikiaye.” Mnaona? Msomaji wa msikilizaji; yule asomaye, na kusikia, amebarikiwa. Kwa hiyo ukiketi tu na kulisikiliza, umebarikiwa. “Heri yeye asomaye, na yeye asikiaye, kwa kuwa wakati umekaribia.”

¹⁵⁷ Sasa, kuanzia 4 hadi 6 ni salamu kwa Kanisa. Sasa tunataka kuchukua hiki cha 4 na cha 6.

¹⁵⁸ Sasa, kabla hatujakifikia, ninataka kila mtu ajaribu kuwazia sana sasa. Ni Kitu gani sasa? Ni ufunuo wa Yesu Kristo, ambapo Mungu aliondoa pazia kutoka kwa wakati. Huu *hapa* wakati, ambao Yesu hangeweza kuuona wakati alipokuwa hapa duniani, zile nyakati za kanisa, kile kingetukia. Kwa hiyo, Mungu aliliondoa pazia, akalivuta nyuma, na kumwacha Yohana aangalie ndani na kuona kile kila wakati wa kanisa utakachofanya, na kuyaandika kwenye kitabu na kuyatuma kwenye yale makanisa saba.

¹⁵⁹ Ni kitu gani? Kristo akifunuliwa katika siku za matendo Ya—Yake. Kimejaa matendo, Kitabu hiki. Pia ni Kitabu cha u—unabii ambao Kristo ameutoa, Mungu ametupa kwa mkono wa malaika Wake, ukaandikwa na Yohana. Na baraka kwa kila mtu atakayeusoma au kuusikia ukisomwa, kwa kuwa—kwa kuwa wakati umekaribia wakati haya yote yametimizwa.

¹⁶⁰ Tuna mandhari nzuri sasa. Pia kumbukeni, tunaliwazia Kanisa. Upande mmoja, Kanisa lilianza; upande huo mwingine, kanisa linaisha. Tutaliingilia kindani zaidi, Jumatatu usiku, tutakapozifikia zile nyakati za kanisa.

Yohana, kwa yale makanisa saba yaliyoko Asia: Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwake yeye aliyeko, . . . aliyekuwako, na atakayekuja; na zitokazo kwa Roho saba zilizoko mbele ya kile kiti cha enzi.

¹⁶¹ Sasa tunafikia kwenye mambo ya kisiri na sehemu zenye kilindi za ile mifano. Kimeandikiwa yale makanisa saba yaliyoko Asia Minor. Yalikuwa—yalikuwa. . . Zile—zile nyakati, wakati huo, zilikuwa zije siku za usoni. Naye aliyatukuza na—na kuyasifu kwa sababu ya kazi zao na yale yaliyokuwa yamefanya. Lakini, sasa, kimeandikiwa hayo makanisa, yale makanisa saba yaliyoko Asia Minor.

162 Sasa, Asia Minor haikuwa ni Asia yote, bara la Asia. Ilikuwa ni sehemu ndogo tu. Wao wanadai, ni mahali yapata ukubwa wa jimbo la Pennsylvania, mnaona, ama kitu kama hicho, ama Indiana; mahali padogo tu ambapo haya makanisa saba yalikuwa. Kulikuwa na makanisa mengi zaidi ya hayo wakati huo. Na, ila, ilionyesha sifa zao. Sasa ninasoma hapa kile nilichopata kutokana na kusoma kwangu historia yake.

163 “Naye ni... Amelaaniwa yeye asikiaye na, ama, asiyeasikia.”

164 Na—na sasa, inafikia kwenye wakati wa kifungu hiki cha 4 ambacho tunataka kuelezea jambo fulani hapa. “Kutoka Kwake aliyekuwako, na aliyeko, na atakayekuja, naye ana Roho saba; kutoka kwa wale Roho saba walioko mbele ya kiti Chake cha enzi.” Sasa, “Hao Roho,” tutawafikia baadaye.

165 Sasa, hapa linaelezea, kama ukiangalia mle—mle ndani. Pia kwenye kifungu cha 7, ama kifungu cha 8, Yeye anarudi tena na kusema, akilielezea tena. Sasa angalieni. Yale makanisa saba yameandikiwa. “Kutoka Kwake aliyeko, aliyekuwako, na atakayekuja. Aliyekuwako, wakati mmoja; aliyeko sasa; na atakayekuja.” Sasa, Yeye anaonyesha hapa ninii Yake yenye sehemu tatu, madhihirisho Yake yenye sehemu tatu ya kazi Yake.

166 Sasa kama utachukua kifungu cha 8. Tutakifikia, katika dakika moja tu. Tutakichukua kifungu cha 8.

*Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na mwisho,
asema Bwana, aliyeko... aliyekuwako, na atakayekuja,
Mwenyezi.*

167 Sasa tunakiangalia kifungu cha 4 na cha 6, vyote viwili ni kitu kimoja. Kimoja, Yeye anasema, “Kwake Yeye aliyekuwako, aliyeko, atakayekuja.” Yeye anajaribu kuweka nini mbele ya Kanisa? Ungu Wake. Siku hizi, watu wanajaribu kumfanya na—nabii. Yeye ni zaidi ya nabii. Na watu wengine wanajaribu kumfanya Miungu watatu. Yeye si Miungu watatu. Yeye ni Mungu mmoja aliyeshi katika ofisi tatu, madhihirisho matatu ya Mungu yeye yule.

168 Sasa, kumbukeni, huu ndio Ufunuo, “Na yeyote asikiaye wala hayashiki maneno ya kitabu hiki, sehemu yake itaondolewa katika kitabu cha uzima.” Yesu hajifunui Mwenyewe kama Miungu watatu, bali Mungu mmoja na ofisi tatu. Loo! Litakolea baada ya kitambo kidogo, tutakapofikia kwenye nyakati hizo za kanisa na kuona walipolipotezea jambo hilo. Lilisababisha mgwanyiko mkubwa kwenye Baraza la Nikea. Wote wawili walivuka mipaka.

169 Nao walifanya jambo lile lile katika siku hizi za mwisho tena, kama vile tu lile Baraza lililotangulia Nikea tena, maana kutakuwako na lingine. Kwa hakika tu kama ninavyosimama hapa, makanisa ya Kikatoliki na ya Kiprotestanti yataunganisha kitu fulani pamoja, ama kukubaliana pamoja. Hebu

mwangalieni askofu mkuu wa Canterbury kule sasa. Hayo yote yanalundikana moja kwa moja pamoja. Wala hakuna fundisho la Miungu watatu katika Biblia. Kuna Mungu mmoja.

¹⁷⁰ Na imefunuliwa hapa katika Kitabu cha Ufunuo, kwamba kitabu chote rasmi cha Maandiko huenda kikathibitishwa hapa, naye Kristo akatia muhuri Wake juu yake. Hiki Ndicho. Kama mtu yeyote akiondoa au kuongezea, huyo ataondolewa katika Kitabu cha Uzima, kwake. Kwa hiyo likaribieni hili sio kwa mawazo finyu, likaribieni hili kwa moyo wazi na nia wazi.

¹⁷¹ Sasa, kwenye Baraza la Nikea, wanafikia maamuzi mawili makubwa. Kwenye. . . Loo, wengi wao katika siku hizo za wale yazee wa kanisa la mwanzoni, walikuwa na maoni mawili yasiyo na kadiri. Moja la hayo lilikuwa ni Mungu wa utatu, wa utatu. Na hilo lingine lilikuwa ni Mungu m—mmoja. Nao wote wawili wakaibuka na wakatoka wakiwa matawi mawili manyofu, yametokeza namna *hiyo*. Utatu ukawa ni mahali pa utu wa miungu watatu. Waumoja wakawa ni umoja, wakiwa wamekosea kadiri tu ya hao wengine. Kwa hiyo wote walienda kombo, bali mumu *Humu* inafunuliwa ile Kweli.

¹⁷² Yesu asingeweza kuwa Baba Yake mwenyewe. Wala, kama alikuwa na Baba nje ya Roho Mtakatifu, basi Yeye ni mwana haramu. Wala sio. . . Roho Mtakatifu alimzaa Yeye, Naye alisema Mungu alikuwa ndiye Baba Yake. Kwa hiyo Roho Mtakatifu na Mungu. . . Hiyo ni Mathayo 1:18. Endapo. . . Roho Mtakatifu na Mungu hawana budi kuwa ni Mtu yule yule, la sivyo Yeye alikuwa na baba wawili. Naye aliitwa *Imanueli*, ambalo ni, “Mungu pamoja nasi.” Yeye alidai, wakati alipokuwa hapa duniani, kwamba Yeye na Baba walikuwa ni Mmoja.

¹⁷³ Nina Maandiko yote yaliyoandikwa hapa kusudi mpate kuyapata, kama tulikuwa na swali hi—hili, ama kitu fulani.

¹⁷⁴ Sasa, wakati alipodhihirishwa hapa, kama ofisi yenye sehemu tatu ya utu Wake, “Yeye aliyekuwako, Yeye aliyeko, Yule atakayekuja, Mwenyezi,” sasa, hakuna Miungu watatu hapo; kuna Mungu mmoja.

¹⁷⁵ Na katika Baraza la Nikea, kufanya jambo hili, kusudi hili litendeke, iliwabidi kuchukua utatu, kwa sababu katika ulimwengu wa Kirumi walikuwa na miungu wengi. Waliomba mababu wao waliokufa. Ninayo hiyo historia papa hapa ambapo tunaweza kuinukuu. Mnaona? Waliomba mababu wao waliokufa. Hiyo ndiyo sababu hao wana Mtakatifu Sisilia, na Mtakatifu Markus, na mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu.

¹⁷⁶ Wakati, Mtume Petro alisema, “Hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na wanadamu, ila Mwanadamu Kristo Yesu.” Mmoja.

¹⁷⁷ Iliwabidi wawe na mungu wa utatu. Kwa hiyo, wa—walikuwa na Jupita, Marsi, Venasi. “Wala haikuwa sawa,

kuwaweka wote katika Mungu mmoja,” kwa hiyo wakampasua tu, nao wakafanya ofisi tatu za Mungu kuwa ni Miungu watatu mbalimbali.

178 Lakini Yeye anasema dhahiri hapa, katika Ufunuo, Yeye ni Nani. “Mimi ni Yeye aliyekuwako, Yeye aliyeko, na Yule atakayekuja, Mwenyezi.” Tatalipata baadaye kidogo hapa, Yeye alisema, “Mimi ni Alfa na Omega,” A mpaka Z, yote, hizo alfabeti za Kiyunani. “Ninyoro ya Mabondeni, Ua la Uwandani; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi.” Yeye ni Mungu, Mungu. “Bil- . . .” Timotheo wa Kwanza 3:16, “Bila ubishi, siri ya utauwa ni kuu: kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na Malaika, akaaminiwa ulimwenguni, akapokelewa juu Utukufuni.” Mungu! Sio mtu wa tatu ama nabii, bali Mungu Mwenyewe, alidhihirishwa katika umbo la kibinadamu. Sasa, huu ni ufunuo, kumbukeni.

179 Sasa, Mungu, hapo mwanzo, alikuwa ni Yehova mkuu aliyeshi katika Nguzo ya Moto, iliyoning’inia juu ya Israeli, na kuwaongoza. Huyo alikuwa ni Mungu, Malaika wa Agano. Alishuka mlimani; mlima wote ukawaka Moto. Moto uliruka kutoka mlimani, na kuandika zile Amri Kumi. Yeye aliitwa “Ubaba wa Mungu,” kwa watoto Wake, jamii Yake ya watu waliochaguliwa, Wayahudi.

180 Ndipo Mungu yuyo huyo alidhihirishwa katika mwili uliozaliwa na bikira ambao aliuumba kwenye tumbo la uzazi la Mariamu, na akaishi na kufanya maskani na kuitandaza hema Yake, tuseme, miongoni mwa wanadamu. Basi Mungu yuyo huyo alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Biblia ilisema hivyo. “Mungu alikuwa ndani ya Kristo.” Mwili ulikuwa ni Yesu. Yesu, “Ndani Yake mlakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.” Huwezi kumfanya watu watatu, sasa. Usibatize kwa Miungu watatu. Kuna Mungu mmoja. Mnaona? Mungu mmoja. Sasa, Mungu yuyu huyu alifanyika mwili.

Yeye alisema, “Nalitoka kwa Mungu, ninaenda kwa Mungu.”

181 Baada ya Yeye kutoweka duniani, kwa mauti Yake, kuzikwa, na kufufuka, na kupaa, Paulo alikutana Naye akienda zake Dameski, wakati angali alikuwa akiitwa “Sauli.” Ndipo Sauti ikaja, na kusema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi Mimi?”

Akasema, “U nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

182 Naye alikuwa ni Nguzo ya Moto, Nuru iliyoyafumba macho ya huyo mtume. Alikuwa amegeuka. Yesu yule yule alikuwa amegeuka akawa Mungu, Baba, tena. Hiyo ndiyo sababu alisema hapa, “Mimi ni Mwenyezi,” katika umbo lile lile alilokuwamo kabla hajafanyika mwili; na mwili Wake alimoishi, ulioitwa Yesu, Mtu tunayemjua, Yesu.

183 Sasa, kama vile wengi wenu wapendwa waumoya mnavyobatiza katika, “Jina la Yesu,” mmekosea. Kuna mamia ya Mayesu ulimwenguni leo hii, bali kuna Bwana Yesu Kristo mmoja tu. Yeye alizaliwa Kristo. Mayesu wengi. Nimekutana na wengi wao. Bali kuna Bwana Yesu Kristo mmoja tu, Yeye ni Mungu.

184 Basi Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu si *majina*. Hizo ni sifa zinazoambatana na Jina moja. Wanabatiza, “Jina la ‘Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.’” *Baba* si jina, na *Mwana* si jina, wala *Roho Mtakatifu* si jina. Ni sifa, kama vile “mwanadamu.” Hivyo ndivyo alivyo, Roho Mtakatifu. Mwanadamu. . . Ama, roho, Roho Mtakatifu. Halafu wanasema, “Katika Jina la ‘Baba.’” Waangalieni akina baba, na wana wa wana wenu. Waangalieni wanadamu walio humu ndani. Mnaona? “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” si jina. Ni sifa inayoambatana na Jina la “Bwana Yesu Kristo.”

185 Hivyo ndivyo lile Kanisa la kimitume lilivyobatiza, hapo mwanzo. Nami nitamwomba mtu yeyote atoe fungu moja la Maandiko, ama wakati mmoja katika historia, ambapo mtu yeyote alipata kubatizwa katika Kanisa la Kikristo kwa njia nyingine yoyote ila katika. . . ila katika Jina la “Yesu Kristo” mpaka kanisa Katoliki lilipoundwa. Nao wakachukua “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” ikawa kanuni ya imani. Sasa ileteni historia yenu, baadhi, wanahistoria. Naam. Hakuna kitu kama hicho. Baada ya 304 A.D., 304, ulitokea ubatizo wa utatu wa Mungu wa utatu, “Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu.” Ni upagani.

186 Kabla juma hili halijakwisha, nitalisoma kutoka kwenye vitabu na kuwaonyesha kwa Biblia. Tunazungumza asubuhi ya leo juu ya Ufunuo, na kuthibitisha mahali ulipoingilia, na jinsi ulivyoanza kuwako. Rudi kwenye ile Kweli, ndugu! Tuko katika siku za mwisho.

187 Ngojeni mpaka tutakapolifikia kanisa hilo la Efeso na kulifananisha na la Laodikia, tuone yaliyotukia kati yao. Mtaona jinsi kitu hicho kilivyojipenyeza ndani. Alipofikia wakati wa Luther, kasema, “Unalo jina kwamba ‘unaishi,’ bali umekufa.” Neno lenyewe *Sardi* linamaanisha “kufa.” Walilipoteza katika ile miaka elfu moja mia tano ya Nyakati za Giza. Kila moja ya makanisa hayo lilidumisha hilo mpaka wakati huo. Ndipo walipofanya lile Baraza la Nikea la 606, kisha wakaliangamiza Jina hilo na kufanya Miungu watatu kutoka Kwake.

188 Yeye alisema hapa, “Mimi Ndimi aliyekuwako, Yeye aliyeko, na atakayekuja, Mwenyezi.” Hakika.

189 Yeye alikuwa na Utu wenye sehemu tatu duniani. Alipokuwa duniani, alikuwa Kiumbe mwenye sehemu tatu. Duniani, alikuwa ni Nabii. Yeye pia Mbinguni, ni Kuhani. Na atakaporudi

duniani tena, Yeye atakuwa ni Mfalme. Nabii, Kuhani, na Mfalme. Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja. “Aliyekuwako,” alikuwa ni Yesu, nabii. “Aliyekuwako sasa,” ni Kuhani, akitoa dhabihu za kiroho, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, na kujifunua Mwenyewe na kuthibitisha ya kwamba Yeye yuko miongoni mwetu. Nabii, Kuhani, na Mfalme, bali Mungu Mmoja.

¹⁹⁰ Wakati alipokuwa duniani, Yeye alikuwa ni Nabii, Neno. “Shahidi mwaminifu,” Biblia inamwita, baadaye kidogo. Shahidi mwaminifu, ni nabii. Yeye alikuwa Kuhani, na wakati. . . Yeye ni Kuhani sasa, na atakapokuja, atakuwa ni Mfalme.

¹⁹¹ Kama mtafungua, msome Ufunuo 15:3, mnaweza kuona katika Ufunuo 15:3. Hebu tufungue hapa tuone yale Yeye. . . kama atakuwa Mfalme, kama Yeye ni Mfalme wakati atakapokuja. Sasa tunaenda kwenye Ufunuo, mlango wa 15 na ki—kifungu cha 3.

Nao waliimba wimbo wa Musa, mtumishi wa Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo, wakisema, Ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa watakatifu.

¹⁹² Yeye alikuwa nini duniani? Nabii. Watu walijuaje kwamba alikuwa ni Nabii? Alifanya ishara ya Masihi, ambaye alikuwa ni Nabii. Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Walimkosaje? Kwa sababu walikuwa wakitazamia kitu kingine. Naye alifanya ishara ya Masihi, wala wasingeisikia. Yeye alikuwa ni Nabii.

¹⁹³ Musa alisema, “Bwana Mungu wenu atawaondokesha Nabii mithili yangu. Itakuwa kama hawatamsikia Nabii huyu, watakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa watu.”

¹⁹⁴ Yeye alikuwa Nabii duniani, sasa, kwa sababu alikuwa ni nini? “Shahidi mwaminifu wa Neno la Mungu.” Amina. Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa.

¹⁹⁵ Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza.

Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, . . .

¹⁹⁶ Yeye alikuwa shahidi wa kweli na mwaminifu kwa Neno la Milele la Mungu. Alikuwa ni Neno, alikuwa ni Neno la Mungu. Na, akiwa ni Neno, Yeye alikuwa ni Nabii. Kwa maana Neno la Mungu lilipitia Kwake. Alikuwa aseme Jambo hilo tu. “Siwezi kufanya lolote kwa nafsi Yangu, bali anayonionyesha Baba kufanya. Si Mimi nizifanyaye hizo kazi. Bali ni Baba anayeishi ndani Yangu, Yeye anazifanya hizo kazi. Mimi na Baba Yangu

ni Mmoja. Baba Yangu yu ndani Yangu,” alisema Yesu, yule Mwanadamu, ile Maskani.

¹⁹⁷ Mungu ana sifa nyingi: Yehova, Yehova-Yire, -Rafa, -Manase. Loo, nyingi! Yeye ana majina saba ambatani, ya ukombozi. Ana sifa nyingi: Ninyoro ya Mabondeni, Ua la Uwandani, Nyota ya Asubuhi; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Yote hayo. Bali ana Jina moja la kibinadamu. Mungu alikuwa na Jina moja tu, na hilo lilikuwa “Bwana Yesu Kristo.”

¹⁹⁸ Wakati alipozaliwa, Kristo, Bwana. Siku nane baadaye, Roho Mtakatifu aliita Jina Lake “Yesu.” Mama Yake alimpeleka akatahiriwe, na kumwita “Yesu.” Alizaliwa Kristo.

¹⁹⁹ Kama vile, nilivyozaliwa Branham. Nilikuwa Branham wakati nilipozaliwa, ndipo nikapewa jina la “William.”

²⁰⁰ Amina. Naye alizaliwa Kristo, Mwokozi. Ndipo alipokuwa na umri wa siku nane, akapewa jina la “Yesu.” Naye alikuwa Bwana wa Utukufu, aliyedhihirishwa. Kwa hiyo, Yeye ni Bwana Yesu Kristo, Mungu wa Utukufu aliyedhihirishwa miongoni mwetu. Loo, Huyo hapo!

²⁰¹ Duniani, Yeye alikuwa ni Nabii. Utukufuni, Yeye ni Kuhani. Ajapo, Yeye ni Mfalme. Loo! Ninapenda hilo.

Nabii, “Shahidi mwaminifu wa Neno.”

Kuhani, “Akiwa na Damu Yake Mwenyewe mbele za Mungu.”

Mfalme, “Mfalme wa watakatifu.” Sio mfalme wa ulimwengu, sasa. Yeye ni Mfalme wa watakatifu. Tunao wafalme wa duniani juu ya hao watu. Lakini tunaye Mfalme, pia, pamoja na Ufalme. Hiyo ndiyo sababu tunatenda tofauti.

²⁰² Kama nilivyosema sio muda mrefu uliopita, kuhusu mke wangu, tulikuwa tukienda hapa dukani nasi tukaona mwujiza, karibu ni mwujiza. Ulikuwa ni msimu wa kiangazi, mwanamke mmoja alikuwa amevaa gauni. Nikasema, “Hilo ni jambo la kigeni.” Nikasema, “Kama ningalikuwa na kamera yangu, ningempiga picha huyo mwanamke.” Mnaona? Kwa sababu sisi. . . Huyo alikuwa ndiye mwanamke wa kwanza tuliyemwona amevaa sketi, mwajua, aliyevaa kama impasavyo mwanamke, wanawake wote.

²⁰³ Akasema, “Vema, ni kwa nini, Bill, kwamba watu wetu wanavaa mavazi, ni kwa kuwa tu—tumeamriwa?”

²⁰⁴ Nikasema, “Sio watu wetu. Ni watu wa Mungu. Watu wa Mungu, wanahitaji utakatifu.”

Kasema, “Vema, hivi hawaendi kanisani?”

²⁰⁵ Nikasema, “Kuna mama mmoja pale *pale*, ambaye huimba kwenye kwaya katika kanisa fulani hapa.”

“Vema, basi, ni kwa nini hivyo?”

206 Nikasema, “Ni kwa sababu hajafunzwa vinginevyo.” Hiyo ni kweli kabisa.

207 Hilo ni kanisa la kimwili, tatalifikia juma hili; Kanisa la kiroho, kanisa la kimwili. Wote wanafuata mkondo wakirudi moja kwa moja kwenye kanisa mama, kama Biblia ilivyosema, katika Ufunuo 17, wangepanya hivyo. Wanarudi huko moja kwa moja, wote, wakifanya kama hilo, wakiunda madhehebu. “Vema, sisi ni ninii *fulani*...Tunaunda dhehebu. Sisi ni *hili* na sisi ni *lile*.” Haikuwa hivyo hapo mwanzo. Wakichukua mamlaka yote kutoka kanisani na kuyaweka juu ya askofu ama papa. Mungu yuko ndani ya Kanisa Lake, miongoni mwa watu Wake, akijidhihirisha Mwenyewe kupitia kwa walei na kila mahali, sasa. Lakini katika siku hii . . .

Akasema, “Vema, hivi sisi si Wamarekani?”

208 Nikasema, “La. Tunaishi hapa, bali sisi si Wamarekani. Sisi ni Wakristo. Ufalme wetu ni wa huko Juu.”

209 Na kama maisha yetu yanatoka Huko juu, basi tunatenda jinsi hiyo. Kwa sababu, tunakuja...Maisha yetu yametoka Mahali patakatifu. Unaonekana tofauti. Unavaa tofauti. Wanawake wa Huko juu wana nywele ndefu. Nao hawapaki nyuso zao rangi. Wala—wala hawavai kaptura. Wana—wanavaa sketi, na majoho marefu na magauni. Nao wana nywele ndefu, na kadhalika. Kwa hiyo ta—tabia yake, inayotoka Huko juu, inaakisi juu yetu.

210 Wanaume hawavuti sigara, kutafuna tumbaku, kusema uongo, kuiba. Wanakuja, roho zao, zinatoka Mahali patakatifu, huwafanya watende kitakatifu, wanafahamiana kama ndugu. Uh-huh. Jambo ndilo hilo.

211 Sisi ni wa Ufalme fulani, nasi tuna Mfalme. Naye ni Mfalme wa watakatifu. Nalo neno *mtakatifu* linatoka kwenye neno “waliotakaswa.” Ndipo mtu anapotakaswa, Kristo, Roho Mtakatifu anaingia moyoni na anakuwa Mfalme juu yao. Loo, jamani! Hilo linapaswa kukolea. Loo! Wakati chombo cha Mungu kilichotakaswa...Kristo, Mfalme, Roho Mtakatifu, anapoingia ndani. Na Yeye...Mfalme ana milki Yake. Amina. Nao utu wako wote unatawaliwa na Mfalme wa watakatifu. Ufalme! Kila ufalme duniani utatikiswa, utaangamizwa na nguvu za atomiki. Bali Biblia inasema, “Tunapokea Ufalme usioweza kutikisika.” Amina. Huyu hapo, Mfalme wa watakatifu.

212 Ninawatakeni muone mifano ya Kristo, pia, katika Biblia na hapa duniani. Duniani, Yeye alikuwa ni Nabii. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nabii ni Neno. Tunajua hilo. Neno *nabii* linamaanisha “mfasiri wa Kiungu wa Neno.” Neno la Kiungu limeandikwa, naye nabii ana Roho ya Kiungu ya Mungu ndani yake. Na, mwajua, nabii katika Agano la Kale aliitwa “mungu.” Ni wangapi walijua hilo?

213 Yesu alisema, “Kama waliwaita miungu... Si imeandikwa katika torati yenu, hao ni... ‘Ninyi ni miungu’? Na ikiwa waliwaita ‘miungu,’ ambao Neno la Mungu liliwajia, nabii, mtanihakumuje Mimi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?”

214 Kwa sababu, alitwa “mungu,” kwa sababu alibeba ndani yake Neno la Mungu, BWANA ASEMA HIVI. Kwa hiyo, neno *nabii* linamaanisha ninii, “fasiri ya—yake haipaswi kuchanganywa.” Mnaona? Kama Mungu... Yeye anasema, “Akitokea mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho, ama nabii, Mimi Bwana nitasema naye. Analosema likitimia, basi msikieni, kwa sababu niko pamoja naye. Lakini kama lisipotimia, basi msimsikie; sijamtuma.” Hivyo ndivyo unavyojua hilo. Halafu basi, unaona, Tafsihi ya Kiungu ya Neno inabidi ilingane na ufunuo huu wa mwisho kwa kanisa.

215 Yeye ni Mungu, Mwenyezi. Duniani, alikuwa ni Nabii, ambaye ni tai. Ni wangapi wanaojua ya kwamba nabii anahesabiwa kuwa ni tai? [Kusanyiko linasema, “Amina.” —Mh.]

216 Tai ndiye ndege mwenye nguvu kuliko wote tuliye naye, mwenye nguvu zaidi. Baadhi ya mabawa yao yananyoka futi kumi na nne, ncha hadi ncha. Anaweza kuchukua na kuruka juu sana hata ndege mwingine yeyote akijaribu kumfuata, angechanganyika, manyoya yangemtoka naye angepasuka vipande. Kwa sababu gani? Yeye ameundwa shesheli. Na inamfaa nini kuruka juu hivyo kama hawezi kuona kile anachofanya wakati akiwa huko juu? Ati wanena kuhusu jicho la mwewe? Unapaswa kuona jicho la tai.

217 Mwewe anaweza, huenda akamwona kuku. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo shida ya baadhi ya hawa mwewe siku hizi. Uh-huh. Lakini, nawaambia, tai huenda hivi kwamba, endapo mwewe alijaribu kumfuata, angekufa. Angepatwa na msongo wa hewa. Hawezi kufika kwenye yale mazingira ambayo tai anafikia.

218 Halafu basi ana jicho, ambapo anaweza kuona mbali sana, wakati akifika huko juu. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu Mungu aliwaita *manabii* Wake, “tai.” Anapanda huko juu, naye ni tai. Anaweza kuona, mbali sana.

219 Naye Kristo, duniani, alikuwa ni Tai. Alipokufa, alikuwa ni Kuhani, kwa hiyo hiyo ilimfanya Mwana-Kondoo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Na wakati atakapokuja tena, Yeye ni Mfalme, kwa hiyo atakuwa ni Simba, amina, Simba wa kabila la Yuda. Amina. Yeye ni Tai, Mwana-Kondoo, na Simba; amina; Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; Nabii, Kuhani, na Mfalme; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja; Mwenyezi; Alfa na Omega, tangu mwanzo hadi mwisho, Mungu wa Milele.

220 Ninataka kuwaulizeni, baadhi yenu ninyi Wakatoliki wa thamani, ambao wanaita hilo, “Uwana wa Milele wa Mungu;

Mungu, uwana wa Milele wa Yesu Kristo pamoja na Mungu.” Mnawezaje kusema neno kama hilo? Mimi ni mpumbavu, nikiwa na elimu ya darasa la saba, bali ninajua vema kuliko hivyo. Neno mwana halina budi kuwa na mwanzo. Kwa hiyo anawezaje kuwa wa Milele na awe ni mwana? Umilele hauna mwanzo wala mwisho. Kwa hivyo, Yeye hawezi kuwa mwana, mwana wa Milele, halafu awe na mwanzo, maana hakuna kitu kama mwana wa Milele. Mwana alikuwa na mwanzo, kwa hiyo hawezi akawa ni wa Milele.

²²¹ Mnaona, Yeye ni Mungu wa Milele, sio mwana wa Milele. Utukufu! Mwenyezi, Yehova-yire, Yehova-rafa, aliyedhihirishwa katika mwili, “Ndani Yake mlíkkaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.”

²²² Na kwenye Siku ya Pentekoste, wakati ile Nguzo ya Moto ilipowashukia watu, mliona, ilijigawa? Nazo ndimi za Moto zikakaa juu ya kila mmoja wao. Moto, kama ndimi, zikikaa juu ya kila mmoja. Mungu alikuwa akifanya nini? Akijigawa Mwenyewe ndani ya Kanisa, miongoni mwa kila mmoja, akiwapa wanawake, wanaume, na hao wote; ilikuwa ni sehemu za Roho Wake, akijigawa Mwenyewe miongoni mwa Kanisa Lake.

²²³ Mtu anawezaje kuja huku na kusema, “Mtu mtakatifu ni papa. Mtu mtakatifu ni askofu?” Mtu Mtakatifu ni Kristo, Roho Mtakatifu ndani yetu. Unawezaje kusema walei hawana neno la kusema? Kila mmoja wenu ana jambo la kusema. Kila mmoja wenu ana kazi ya kufanya. Kila mmoja wenu hana budi kubeba Ujumbe. Utukufu!

²²⁴ Roho Mtakatifu alijigawa kwenye Siku ya Pentekoste. Mungu, akijigawa Mwenyewe. “Siku hiyo mtajua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.”

²²⁵ “Siku hiyo,” Roho Mtakatifu, “juu ya wote, ndani ya wote, kupitia kwa wote.” Amina. Hilo hapo. Roho Mtakatifu ana haki ya kwenda mahali popote atakapo, juu ya mtu yeyote atakaye. Haikulazimu kuchukua yale askofu fulani ama kasisi fulani asemayo. Yeye ndiye Kuhani wetu pekee, kweli, Kuhani Mkuu. Sasa: Nabii, Kuhani, na Mfalme.

²²⁶ Sasa:

Na . . . Yesu Kristo, ambaye ni shahidi mwaminifu, . . . mzaliwa wa kwanza katika wafu, . . . (Tutalifikia hilo) . . . na mtawala wa wafalme wa nchi. Kwake yeye aliyetupenda, na kutuosha na dhambi zetu katika damu yake mwenyewe,

²²⁷ Neno kuoshwa hapo, kwa kweli, katika Kiyunani, linamaanisha “kufunguliwa.” Alitufungulia kutoka kwenye ninii yetu. . . Tulikuwa tumefungwa duniani, na dhambi zetu. Tusingeweza kuona, tusingeweza kusikia, hatukuwa na dhana

ya Mbingu wala chochote kile. Lakini wakati ile Damu iliposhuka chini, iliukata ule ukanda nasi tukafunguliwa. Loo!

228 Nilisoma hadithi wakati mmoja, ni . . . inaweza kuenea hapa vizuri. Mkulima mmoja alimnasa kunguru na kumfunga. Naye akasema, “Nitawapa fundisho hao kunguru wengine.” Kwa hivyo akamfunga maskini huyo kunguru, na mguuni, kwa kamba, ndipo maskini kitu hicho nusura kife kwa njaa. Alikuwa mnyonge sana, ilikuwa ni vigumu kwake kutembea.

229 Hivyo ndivyo, baadhi ya madhehebu haya na makanisa, yamewafunga watu sana. “Huwezi kamwe! Vema, *huu* ndio umbali wote unaoweza kwenda. Siku za miujiza zimepita.” Naam. Wewe umefungwa tu. Hivyo tu. “Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu. Yeye haneni kwa lugha kama alivyozoea kufanya.”

230 Yeye ni Mungu. “Yeye ni yeye yule tu jana, leo, na hata milele,” Waebrania 13:8, akiishi katika makanisa yote. Tatalifikia baada ya mandhari ya asubuhi ya leo. Mnaona? Yeye ni Mungu, anayeishi katika kila wakati wa kanisa. Yeye ataishi katika kila wakati wa kanisa, na ataishi ndani ya watu Wake kama . . . Milele. Kwa kuwa tunao sasa, ndani yetu, Uzima wa Milele.

231 Kwa hiyo, dhehebu hili lilikuwa limemfunga kabisa, mnaona, “Vema, siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.” Maskini jamaa huyo alichechemaa hata akawa mnyonge sana ilikuwa ni vigumu kutembea.

232 Ndipo ikawa siku moja mtu mzuri alipitia hapo, na akasema, “Unajua, maskini kunguru yule, ninamhurumia sana. Hata hivyo, huenda alikuwa akitafuta mahindi yake, lakini hiyo ndiyo njia pekee anayojipatia riziki. Hana budi kupata chakula. Kwa hiyo hakujua vinginevyo, yeye yuko huko nje tu akitafuta nafaka. Kwa hiyo kama . . .” Basi alichukua ninii yake . . . ndipo akachukua kisu chake na kumfungulia maskini kunguru huyo.

233 Nanyi mwajua, hawa hapa wakaja hao kunguru wengine, wakaja pale, wakasema, “Hima, Kunguru Johnny. Hima twende Kusini. Hali ya baridi inakuja.”

234 Mnajua nini? Huyu kunguru angeenda tu umbali alioweza kwenda huko nje. Akasema, “Siwezi kufanya hivyo. Si, si kwa ajili yetu siku hizi. Kamwe ha—hatuwezi kufanya hivyo.” Mnaona? Alikuwa amefungwa kwa muda mrefu sana, hata alifikiri alikuwa angali amefungwa. Mnaona?

235 Na hivyo ndivyo ilivyo na watu wengi, mmefungwa sana na kanuni za imani na madhehebu, kutoka kwa maskini yule mama kahaba wa kale huko nyuma, akiwaambia, kwamba, “Yesu Kristo si yeye yule. Wala hakuna kitu kama uponyaji. Hakuna ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hakuna upuuzi kama huo.” Akijaribu kuwaambia ninyi hayo. Mmefungwa kwa muda mrefu sana hata mngali mnafikiri mmefungwa.

236 Mtu mwema, Kristo, alitoa Damu Yake apate kutusafisha na kutufungulia kutoka kwenye dhambi zetu. Dhambi ni kitu gani? Nitamwomba mtu yeyote aniambie. Dhambi ni nini? *Dhambi* ni “kutokuamini.” Hiyo ni kweli. “Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari.”

237 Nayo dhambi yako ndicho kitu pekee kinachokuzuia usiwe huru. Ni kwa sababu Mungu alikukatilia mbali na kutokuamini kwako, bali umefungwa sana na kanuni za imani hata ungali unafikiri umefungwa. Unakufa tu kwa njaa, unaona, ukienda kwa kuchechemaa, “Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Wananiambia (Mimi ni wa Church of Christ), ‘Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho.’”

238 Ewe maskini kunguru anayekufa kwa njaa! Mbona usije asubuhi ya leo? Kwa nini usiruke uende? Haleluya! “Inuka kwa mabawa asubuhi, uruke uende kwenye Jua la Haki, lenye uponyaji katika mbawa Zake.” Amina. Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo, ndugu, dada. Loo! “Yeye ambaye Mwana amemkatilia mbali akawa huru, ni huru kweli.” Naam, bwana!

239 “Vema, mchungaji wangu. . .” Hakuna kitu kuhusu hilo. Biblia ilisema, “Uko huru.” Hiyo ni kweli. Uko huru.

“Kanisa langu. . .”

240 Vema, katiliwa mbali uwe huru. “Ametuosha na kutufungulia kutoka kwenye madhehebu yetu, katika Damu Yake Mwenyewe,” na ametufanya huru tupate kujiwazia wenyewe, na kujitendea wenyewe, na kujitetea wenyewe, na kujishughulikia wenyewe.

241 “Vema, kama ningalirudi na kumwambia mchungaji wangu ilinibidi kubatizwa tena, yeye angeninii. . .”

242 Vipi kuhusu, “Uko huru”? Huu ni ufunuo, mwajua. Vema. Uko huru.

243 Kama umenyunyiziwa chumvi kidogo ya kutikisa namna *hii*, jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” hiki hapa kidimbwi, tayari asubuhi ya leo, kikiwa na maji ndani yake. Unaona? Naam, bwana. Si sawa.

244 Kwa hiyo, hujafungwa tena. Uko huru, bali labda hujui hilo. Lakini hebu niwaambie asubuhi ya leo, Biblia ilisema, “Alitufungulia kutoka kwa dhambi zetu, kutokuamini kwetu, tupate kuupokea Ufunuo wa Yesu Kristo.” Nenda zako, huru! . . . inabidi uchukue yale kanisa lolote lisemayo juu Yake. Chukua kile Mungu alichosema juu Yake. Huu hapa Ufunuo Wake ukifunua Yeye ni Nani.

245 “Daima niliamini ya kwamba Mungu Baba alikuwa na ndevu ndefu, nywele nyeupe; naye Mwana alikuwa ni mtu wa makamu; naye Roho Mtakatifu alikuwa ni mleta bahati.” Ndugu, huo ni upagani. Huo ni upagani endapo unaamini katika Miungu watatu.

246 Amri ya kwanza kabisa, je, Amri ya kwanza ni ipi? “Sikilizeni, Enyi Israeli: Mimi ni BWANA Mungu wenu, Mungu mmoja.” Jambo ndilo hilo.

247 Yeye ni Mungu mmoja, sio miungu watatu. Aliishi katika ofisi tatu, akatumika mahali patatu. Yeye ni Nabii, Kuhani, na Mfalme. Yeye ni Tai, Mwana-Kondoo, na—na Simba. Yeye ni Ninyoro ya Bondeni, Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni, na Nyota ya Asubuhi, Shina na Mzao wa Daudi. Yeye ni kuanzia A mpaka Z. Yeye ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Yeye ni yote hayo, bali Yeye ni Mmoja. Yeye ni Mungu mmoja. Hizo ndizo sifa Zake zinazomwendea Yeye, lakini kuna Mungu mmoja.

248 Kamwe hakukuwa na mtu, ukurasa wowote wa Biblia wala katika historia, mpaka kufikia kanisa Katoliki, aliyewahi kubatizwa kwa kuzamishwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.”

249 Kama ukinionyesha ukurasa huo ama chochote kile, liandike, uniwekee hapa, usiku wa leo, nami nitatoka kwenye kanisa hili, nikisema, “Mimi ni mnafiki; nimewafundisha watu uongo.” Kama unaweza kunionyesha fungu moja la Maandiko, ama kuniletea historia moja, historia ya kweli, itakayionyesha ambapo watu walipata kubatizwa, katika Biblia, katika jina la “Baba, Mwana, Roho mtakatifu.” Ama, uniletee Andi- . . . ama, kitabu kimoja cha historia, ukurasa mmoja, nukuu moja katika historia, ambapo mtu yeyote alipata kubatizwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” mpaka kwenye lile Baraza la Nikea la kanisa Katoliki. Njoo, niletee mimi; nami nitajibandika tangazo mgongoni mwangu na kutembea kote Jeffersonville, nawe ukifuata nyuma na baragumu, ukiipiga. Nitaandika hapo, “Nabii wa uongo, anayewapoteza watu.”

250 Na, mchungaji, kama upo hapa asubuhi ya leo, ungefanya hivyo, unapaswa kuniruhusu nikufanyie hilo. Unaona? Njoo, ukanionyeshe. Lakini unaogopa.

251 Sasa, ni kitu gani? *Huu* ndio Ufunuo. *Huu* ndio Ufunuo. Naye huyu ni Roho Mtakatifu, Kristo, akituma Ujumbe Wake kwa makanisa. Usikieni. Usikieni. Hivyo ndivyo Biblia inavyofundisha.

252 Uliingilia wapi? Kama tu hamtakasirika, muondoke, juma zima, chu—chukueni Mabaraza ya Nikea. Chukueni *Babeli Mbili* kilichoandikwa na Hislop. Chukueni . . .

253 Sasa, historia ya Josephus ni sawa, lakini aliandika tu aya moja juu ya Kristo, kasema, “Palikuwapo na mtu mmoja aliyetwa Yesu aliyezunguka-zunguka huku, akiwaponya watu. Na—naye akafa, wala, sivyo, Pilato alimwua, na—na, ama Herode, ama akamwua. Ndipo wanafunzi wakaenda wakaiba mwili wake, wakauficha. Ndipo basi kila usiku walienda na kukata kipande chake na kuula.” Kasema, “Walikuwa

wala watu.” Kwa hiyo, walikuwa wakifanya ushirika, mnaona. Mawazo ya kimwili! Josephus si mtu wa kusikilizwa.

254 Lakini hebu chukua *Kitabu Cha Wafia Imani cha Foxe*. Hicho hapo kizuri na cha kweli. *Kitabu Cha Wafia Imani cha Foxe*, ni wangapi waliopata kukisoma? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. *Nyakati Za Mwanzoni* cha Pember, ama—ama *Babeli Mbili* cha Hislop, ama—ama baadhi ya vya kweli. Ama, ki—kile maarufu sana tulicho nacho ni cha Baraza la Nikea, Baraza lililotangulia Nikea na Baraza la Nikea. Nanyi mnaona pale, huo kamwe haukutajwa, hakuna watu.

255 Yachukue Maandiko Matakatiifu uone kama kulipata kuwapo na mtu yeyote katika Biblia aliyewahi kubatizwa, wakitumia sifa hizo, jina “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Linaonyesha miungu watatu. Ni kwa ajili ya sherehe ya kipagani. Nao Ukatoliki si kitu kingine ulimwenguni ila sursura ya kipagani ya Ukristo. Na kutoka kwa kanisa Katoliki walikuja Martin Luther, John Wesley, Baptisti, Presbiteri, na kadhalika.

256 Lakini katika siku za mwisho kulikuwako na mlango uliowekwa katikati ya hapo, ulioifungua ile Kweli tena, kwamba, “Biblia ilisema hivyo,” na yule nabii mkuu atakayekuja duniani katika siku za mwisho. Nasi tunaamini ya kwamba anakuja. Angalieni. Naye atakuwa na Kanisa. Sasa, tutaona jambo hili sasa.

257 Sasa—sasa, kumbukeni, huu ndio Ufunuo. Huwezi kuondoa Kwake. Sasa, ni changamoto jinsi gani! Mtafute mtu mmoja katika Biblia, mahali pamoja walipopata kumbatiza mtu yeyote katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” au hata kumnyunyizia mtu yeyote, tafuta hilo katika Biblia, kwa ondoleo la dhambi zao. Kamwe hawakufanya hivyo. Na kila mtu, haijalishi jinsi walivyobatizwa, ilimbidi aje na kubatizwa, mara nyingine tena, katika Jina la “Yesu Kristo,” apate Roho Mtakatifu.

258 Matendo 19, “Paulo alipita kati ya nchi za juu za Efeso, akawakuta wanafunzi fulani.” Akasema... Wanafunzi, wanafanya mkutano mkubwa. Walikuwa wakimfuata mtu mmoja jina lake Apolo, ambaye alikuwa ni mwanasheria aliyeongoka; Mbaptisti aliyemwamini Yohana Mbatizaji, naye alikuwa akithibitisha kwa Maandiko ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo.

259 Paulo alipitia hapo na kumwona Akila na Prisila, katika mlango wa 18 wa Matendo. Ndipo akaenda huko kula chakula cha jioni, ama kitu kama hicho, pamoja na Akila na Prisila. Wakamwambia juu ya mtu huyu mashuhuri. Wakaenda kumsikiliza. Akamsikiliza usiku huo. Akasema, “Yeye yuko sawa kabisa. Hilo ni sawa kabisa. Hilo ni zuri. Lakini,” kasema, “je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mliipoamini?”

260 Vipi kuhusu maskini ninyi Wabaptisti huko nyuma, mnaoamini unampokea Roho Mtakatifu *wakati* unapaoamini?

Yeye alisema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?”

Mtu fulani alisema, “Hilo halikuandikwa humo.”

261 Ninakataa hilo. Nina Kiyunani halisi papa hapa, Kiebrania, pia. Biblia inasema katika Kiyunani, na zote mbili, Kiebrania, na pia katika Kiaramu. Katika hizo zote tatu, ninazo papa hapa, zilizosema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?” Hiyo ni kweli. “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?”

262 Sasa, yeye alisema, “Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu yeyote.”

Ndipo akasema, “Mlibatizwa kwa ubatizo gani?”

263 Wakasema, “Tayari tumebatizwa na mtu aliyembatiza Bwana Yesu Kristo. Tumebatizwa katika ubatizo wa Yohana,” shimo lile lile la maji, labda, “mtu yule yule.”

264 Paulo akasema, “Hilo halitafaa kitu. Yeye alibatiza tu kwa toba, sio kwa ondoleo la dhambi.”

265 Sasa, baadhi yenu Waumoja mnakuja huku na—na kubatiza hivyo, hilo ni kosa. Mnabatiza katika, kwa ajili ya wokovu. Maji hayamwokoi mtu; ni Damu, toba. Sio kupitia ubatizo ili kuongoka. La, bwana. Kuongoka huja kwa njia ya Roho. Ubatizo ni—ni onyesho la nje la kazi ya ndani ya wongofu ambayo imefanyika. Mnaona? Vema. Angalieni.

266 Yeye alisema, “Mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?” Wakasema . . .

Akasema, “Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu yeyote.”

Akasema, “Mlibatizwa namna gani?”

Kasema, “Tumebatizwa na Yohana.”

267 Akasema, “Yohana kweli alibatiza kwa ajili ya toba, kwa toba, akisema ya kwamba ‘inawapasa kumwamini Yeye,’ Mwana-Kondoo, Dhabihu itakayokuja, kumwamini Bwana Yesu Kristo.” Basi waliposikia haya, walibatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo. Ndipo Paulo akaweka mikono yake juu yao nao wakampokea Roho Mtakatifu, wakasema kwa lugha na kutabiri.

268 Niambie hayo si Maandiko, na unionyeshe mahali popote, ambapo mtu yeyote alipata kubatizwa kwa njia nyingine yoyote katika Agano Jipya ila kwa Jina la Bwana Yesu Kristo. Nionyeshe.

269 Mtakatifu Agabo na wengi, kulikuwako na wengine, walioendelea kubatizwa hata kufikia wakati wa—wa—wa Baraza la Nikea, na kila mmoja wao alibatizwa katika Jina

la Yesu Kristo. Wamishenari walilima mashamba kwa Jina la Yesu Kristo.

²⁷⁰ Lakini wakati lile Baraza la Nikea lilipokuja, iliwabidi kuwa na miungu watatu. Walimshusha Paulo . . . ama walishusha Jupita, na kumwinua Paulo. Walishusha Venasi, na kumwinua Mariamu. Walikuwa na kila namna ya miungu, kila namna ya watakatifu na kadhalika, kisha wakafanya ubatizo wa utatu na kuwalisha Waprotestanti huo. Nao wangali wanaumeza.

²⁷¹ Bali Nuru za jioni zimekuja sasa. Nabii alisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.”

Ita—itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata;
Katika njia ya maji, hiyo ndiyo Nuru siku hizi,
Kuzikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia ndani;
Nuru za jioni zimekuja,
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

²⁷² Mnaamini Hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, “Na ijulikane, kwenu, enyi nyumba ya Israeli, ya kwamba Mungu amemfanya Yesu yuyu huyu, mliyemsulubisha, kuwa Bwana na Kristo pia;” kifungu cha 16 cha mlango wa 2. Naam. “Mungu amemfanya Yesu yuyu huyu, mliyemsulubisha, kuwa Bwana na Kristo pia. Nyumba yote ya Israeli na wajue, yakini.”

²⁷³ Nilizungumza na Myahudi si muda mrefu uliopita, hapa juu kwenye Nyumba ya Daudi, akasema, “Ninyi Wamataifa hamwezi kumkata-kata Mungu katika vipande vitatu na kumpa Myahudi. Tunajua bora zaidi ya hilo.”

²⁷⁴ Nikasema, “Jambo ndilo hilo tu, Rabi. Sisi hatumkati Mungu katika vipande vitatu.” Nikasema, “Je, unawaamini manabii?”

Akasema, “Hakika.”

Nikasema, “Je, unaamini Isaya 9:6?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Je, nabii alikuwa akizungumza juu ya nani?”

“Masih.”

Nikasema, “Masih atakuwa na uhusiano gani na Mungu?”

Akasema, “Atakuwa ni Mungu.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.” Amina.

Unaona, haya basi. Mnaona, huwezi kumkata-kata katika vipande vitatu.

²⁷⁵ Ikiwa ninyi wamishenari hapa . . . Mmoja wao anaenda hapa kwa Wayahudi, ninaamini, mtu huyu anayeketi *hapa*. Kamwe usijaribu kumpa Myahudi “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.”

Yeye atakwambia upesi sana, anajua mahali lilipotoka, “Baraza la Nikea.” Hatasikiliza hilo. Lakini mwache aone ambapo Mungu huyo alifanyika mwili, Naye ndiye Mungu pekee aliyeko. Mungu, aliyefanyika mwili katika umbo la mwanadamu na kuishi miongoni mwetu, kututakasa; akaondoka, kusudi Yeye Mwenyewe aweze kuja katika umbo la Roho Mtakatifu. Mungu, Baba, Roho Mtakatifu, ni Mtu yule yule.

²⁷⁶ Biblia ilisema katika—katika ukoo wa Yesu Kristo, katika mlango wa kwanza wa Mathayo, Hiyo ilisema, “Ibrahimu alimzaa Isaka. Isaka akamzaa Yakobo.” Na kuendelea, kasema, halafu basi katika . . . Hebu niisome, na ndipo sasa mtajua yale ninayonena habari zake. Mathayo, mlango wa kwanza. Nasi tutaninii . . . Sasa hebu tuanzie kwenye kifungu cha 18.

Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Hivi . . . Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa . . .

²⁷⁷ “Mungu Baba”? Hilo linasema hivyo? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Alionekana ana Mimba kwa uweza wa Nani? [“Roho Mtakatifu.”] Ninii . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] Nilidhani Mungu Baba alikuwa ndiye baba Yake? Basi, Mungu, Baba na Roho Mtakatifu, ni Roho yule yule, la sivyo Yeye alikuwa na baba wawili.

Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, . . . asitake kumwaibisha, aliazimu . . . kumwacha kwa siri.

Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu . . . kumchukua Mariamu mkeo: maana mimba yake ni kwa uweza wa . . .

²⁷⁸ “Mungu Baba”? Aha? [Kusanyiko linasema, “La. ‘Roho Mtakatifu.’”—Mh.] “Roho Mtakatifu.” Basi Baba ya Yesu Kristo alikuwa ni nani? [“Roho Mtakatifu.”] Roho Mtakatifu. Ni nini Hicho kilicho ndani yako? [“Roho Mtakatifu.”] Vema, huyo ni Mungu, Baba, pia. Sivyo? [“Amina.”] Hakika.

Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake YESU: . . .

²⁷⁹ Huyu *hapa* Mungu Baba, huyu *hapa* Mungu Roho Mtakatifu, na huyu *hapa* Mungu Mwana, mnaona, hao ni Miungu watatu. Biblia haisemi hivyo. Hawa wawili hawana budi kuwa ni mmoja, la sivyo Yeye alikuwa na baba wawili. Mnaona? Hawezi kuwa na baba wawili. Mnajua hilo.

Sasa, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake YESU: maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.

Hayo yote yalikuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema,

. . . bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake Imanueli, ambayo maana yake, Mungu pamoja nasi.

280 Huo ni mlango wa kwanza wa Mathayo.

281 Mathayo 28:19, ambapo Yesu alisema, “Nendeni, mkabatize katika Jina Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu ni lipi? [Kusanyiko linasema, “Yesu Kristo.”—Mh.] Yesu Kristo, bila shaka.

282 Ukisoma hadithi ya mapenzi, ikasema, “Yohana na Mariamu wakaishi kwa furaha daima baadaye.” Yohana na Mariamu ni nani? Rudi mwanzoni mwa hadithi hiyo, upate kujua.

283 Iwapo hakuna kitu kama hicho, hakuna jina, “Baba, Mwana, wala Roho Mtakatifu,” basi ni Nani, ni Jina la Nani? Rudi, mwanzoni mwa hadithi hiyo, uone ni Nani aliyekuwa akisema habari zake.

284 Petro, kwenye Siku ya Pentekoste, alisema “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la ‘Yesu Kristo’ kwa ondoleo la dhambi.” Alikuwa na ufunuo.

Yohana alikuwa na ufunuo.

285 Yesu *alikuwa* ndiye Ufunuo, Yeye alijitoa papa hapa kwenye Maandiko, “Mimi Ndimi aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja, Mwenyezi.” Whiu! Vema.

286 Sasa, hebu twende kwenye kifungu cha 7, upesi sana sasa, kabla hatujatoka, upesi tu tuwezavyo. Mwenyezi.

. . . uku- . . . utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele. Amina.

Na . . . kutufanya wafalme na makuhani kwa Mungu . . . Baba yake; basi utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele. Amina.

287 Unaona huo ufunuo hapo, jinsi ulivyofunuliwa? Jinsi ambavyo Mungu . . . Watu hukuna vichwa vyao na kuvuta nywele zao, na kadhalika, wakijaribu kutafuta kujua “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu” ni, kuwafanya watatu, katika mmoja.

Usivute nywele zako na kukikwaruza kichwa chako. Angalia tu juu. Ufunuo hutoka Juu. Na hiyo ni kweli. Yeye atafunua, sio “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Ni ofisi tatu ambamo Mungu mmoja aliishi ndani yake.

288 Alikuwa katika ofisi, “Roho,” akiwa peke Yake, kwa sababu mwanadamu ni kujishusha hadhi, ndipo akajifanyia Mwenyewe mwili, akaishi ndani yake, apate kutoa Damu Yake Mwenyewe; sio kwa kujuana kimwili, kama ilivyokuwa katika bustani ya Edeni, bali kutoa mwili mwumbaji. Na kupitia kwa mwili huo uliozaliwa na bikira, Yeye alitoka Damu iliyotutakasa na

kutufungua kutoka kwa kutokuamini kwetu, tupate kumwamini Yeye. Ndipo, tunapofanya hivyo, tunampokea moyoni mwetu, huyo ni Mungu ndani yetu; Mungu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Mnaona? Kama tu vile Nabii, Kuhani, na Mfalme, hicho ni kitu kile kile. Vema.

289 Sasa, kifungu cha 7, hili ni tangazo. Tangazo ni kwamba:

Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, . . . hao pia waliomchoma: na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake.

290 Loo! Tuna muda kiasi gani? Hilo ni zuri hapo. Mngeweza kuvumilia dakika zingine thela- . . . ishirini? [Kusanyiko linasema, “Naam.”—Mh.] Mngeweza? [“Amina.”] Vema. Sasa, basi, kesho . . . Usiku wa leo, tutajaribu kushika hayo mengine ya *Ono La Patimo*, usiku wa leo. Leo hii, tutamalizia kwenye lile tangazo.

291 Loo! Mnajisikia vizuri? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaipenda Biblia hii ya kale? [“Amina.”] Ni Ufunuo. Ni, ni kitu gani? Mungu ananyosha mkono, katika Kitabu hiki, na kuliondoa pazia, kasema, “Huyo hapo: Nabii, Kuhani, Mfalme; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja. Vitu hivi vyote, ni Mungu.”

292 Sasa, hebu na tuondolee mbali pazia, kwa dakika chache sasa, Bwana akitusaidia, tuliondoe pazia machoni mwetu. Na kupata . . .

Tazama, yuaja na mawingu; . . .

293 Sasa, Yeye anakujaje? “Na mawingu.” Ni wingu la aina gani? Mawingu ya utukufu. Sio moja ya hizi radi, mawingu ya mvua, bali mawingu ya utukufu.

294 Mtaangalia ni wingu la aina gani alilokuwa amefunikwa nalo wakati Petro na hao wengine walipoona ono Lake kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, wingu lilimfunika. Vazi Lake likaangaza. Alikuwa amefunikwa na wingu, nguvu za Mungu.

295 Loo, tatalifikia hilo, hapa katika nyakati hizi za kanisa. Ninawaambia, lina—linafurahisha tu utu wangu wa ndani kabisa, kuliwazia. Kile kuja Kwake . . . Ninaiona siku hii ambayo tunaishi, ambapo hakuna kitu, hakuna matumaini yaliyosalia ila Kuja Kwake.

296 Sasa tatalipata hili upesi. Sasa kumbukeni.

. . . kila jicho litamwona, . . .

297 Sasa, huo haukuwa ni Unyakuo, basi. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Mnaona? Haukuwa ni Unyakuo. Haukuwa ni Unyakuo. Yeye alikuwa akizungumzia nini? Kuja mara ya pili.

. . . na hao waliomchoma: na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake.

298 Sasa tutarudi na kupata historia kidogo. Hebu turudi kwenye Zekaria, na tufungue mlango wa 12 wa Zekaria. Zekaria. Vema.

299 “Naye Bwana akaongeza kwa kanisa kila siku wale waliookoka.” Jinsi tulivyo na shukrani kwa ajili ya ufunuo mzuri wa Yesu Kristo! Hivi hamna furaha kwa ajili Yake? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, tutaweka haya kwenye kitabu upesi tuwezavyo, kwa watu, ndipo mnaweza kukipata, mkisome kwa utulivu chumbani mwenu na kadhalika, na kukisoma kabisa, wewe mwenyewe. Vema.

300 Zekaria, Zekaria, mlango wa 12 sasa wa Zekaria. Nasi tunataka, kuuchukua huu kwa njia ya maombi sana sasa. Nami ninataka kupata hili kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa, Zekaria 12, hebu tuanzie kwenye kifungu cha 9. Sikilizeni kwa makini sasa. Yeye anazungumza juu ya kule Kuja. Zekaria 12, nasi tutaanzia kwenye cha 9, katika kifungu cha 9.

Hata itakuwa . . .

Zekaria, akitabiri, miaka mia nne na themanini na saba kabla ya kuja kwa Kristo.

Hata itakuwa siku hiyo, ya kwamba nitatafuta kuyaangamiza mataifa . . . yote watakaokuja kupigana na Yerusalemu. (Wazia hilo.)

Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba: nao watanitazama mimi ambaye walimchoma, . . .

301 Sasa, Injili inarudi lini kwa Wayahudi? Hapo siku ya Mataifa itakapokwisha, Injili iko tayari, kwenda kwa Wayahudi. Loo, ningeweza, laiti ningaliwabashiria jambo fulani dogo linalokaribia kutukia papa hapa, mnaona, moja kwa moja katika siku hii. Mnaona? Liko karibu kutukia. Tutalipata katika Wakati wa Kanisa. Nalo jambo hili kuu linalokaribia kutokea, litaendelea hata kwenye Ufunuo 11 na kuwachukua hao manabii wawili, Eliya na Musa wakirudi tena kwa ajili ya Wayahudi. Tuko tayari kwa ajili ya jambo hilo. Kila kitu kimekaa katika utaratibu, tayari kabisa. Ujumbe huu wa Mataifa, kama vile Wayahudi walivyuleta kwa Mataifa, Mataifa wataurudisha moja kwa moja kwa Wayahudi tena. Nao Unyakuo utakuja.

302 Sasa kumbukeni, hii hapa inakuja, baada ya ile Dhiki . . . Kanisa halitapitia kwenye ile Dhiki. Tunajua hilo. Biblia inasema hivyo. Mnaona? Vema.

303 Sasa, Yeye atamwaga juu ya nyumba ya Israeli, (kitu gani?) Roho Mtakatifu yule yule, mnaona, baada ya kuondoka kwa Kanisa la Kimataifa.

. . . nao wanitazama mimi ambaye walimchoma, nao watawombolezea, kama vile mtu amwombolezavyo mwanawe wa pekee, nao wataona uchungu kwa ajili

yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza.

Na katika siku hiyo kutakuwa . . . maombolezo makuu huko Yerusalemu, . . . na maombolezo . . . katika—katika bonde la Megido.

Nayo—nayo nchi itaomboleza, kila jamaa peke yake; jamaa ya nyumba ya Daudi peke yao, na . . . jamaa ya nyumba ya Nathani peke yao, na kila moja ya nyumba hizi peke yao; (wakati watakapoona, yatakayotokea, yatakayotukia wakati Yeye atakapokuja kwa mawingu ya utukufu, katika kuonekana Kwake mara ya pili.)

³⁰⁴ Ndipo wakati hao Wayahudi ambao walimchoma . . . Mwajua, Maandiko mengine yanasema watamwuliza, alipata wapi majeraha haya.

Akasema, “Katika nyumba ya rafiki Yangu.”

³⁰⁵ Na hautakuwa tu ni wakati wa maombolezo kwa Wayahudi waliomkataa, kama Masihi, bali itakuwa ni wakati wa maombolezo kwa hao Mataifa walioachwa huko nyuma, ambao wamekubali . . . ambao wamemkataa kama Masihi wao wa siku hizi. Watakuwa wakiomboleza na kulia. Mwanamwali aliyelala atakuwa analia. Hilo ni kanisa lililokataa kupata Mafuta katika taa yake. Kulikuwako na wanawali kumi waliotoka, wote wakiwa ni watu wazuri, lakini watano kati yao walikuwa na Mafuta kwenye taa zao. Hao wengine watano walikuwa ni watu wazuri, watu wazuri, bali walikosa kuwa na Mafuta katika taa zao. “Nao wakatupwa kwenye giza la nje ambako kutakuwa na kilio, kuomboleza, na kusaga meno.”

³⁰⁶ Hili hapa, “Watakuwa wanalia.” Biblia ilisema hapa, “Watakuwa wakilia, na kuvunjika mioyo sana, mpaka hata . . .”

³⁰⁷ Hapa, nitawapa lingine, Mwanzo 45, kama mkitaka kufikia hilo. Hebu tuliendee kwa dakika moja tu na kusoma hayo pia katika Mwanzo, ninii . . . ninaamini, cha mlango wa 45 wa Mwanzo. Ningetaka kupata hili hapa, Yusufu akijitambulisha kwa—kwa watu wake. Nasi tatalipata hili, kuonyesha tu mi—mifano ya yale yatakayotukia katika siku hiyo, ndipo tutayafunganisha pamoja.

Hapo Yusufu hakuweza kujizuia mbele yao . . . waliosimama karibu naye; akapiga kelele, na kusema, Mwondoeni kila mtu . . . mbele yangu.

³⁰⁸ Sasa kumbukeni, Yusufu, akijitambulisha mwenyewe, alipiga kelele, “Kila mtu aondoke mbele yangu.”

Wala hakusimama mtu pamoja naye, Yusufu alipojitambulisha kwa nduguze.

Akapaza sauti yake akalia: nao Wamisri na nyumba ya Farao wakamsikia. (Hapana budi alipiga kelele sana.)

Yusufu akawaambia ndugu zake, Mimi ndimi Yusufu; baba yangu angali hai bado? Wala ndugu zake hawakuweza kumjibu; maana waliingiwa na hofu mbele yake.

Yusufu akawaambia ndugu zake, Songeeni karibu . . . nami, tafadhali. Basi, wakakaribia. Akasema, Mimi ni Yusufu, ndugu yenu, ambaye . . . yule mliye—yule mliyeniuza kwenda Misri.

Basi sasa, msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwamba mmeniuza huku; maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu. (Loo, ni zuri jinsi gani!)

Kwa maana miaka hii miwili imeninii . . . njaa imekuwa katika nchi: na . . . itakuwa, isiyo na kulima wala kuvuna.

Mungu alinipeleka mbele yenu kuwahifadhi masazo katika nchi, na kuwaokoa ninyi kwa wokovu mkuu.

³⁰⁹ Hebu nichukue tu sasa na kulinganisha hayo na Zekaria, wa 12, kwa dakika moja tu. Sasa, tunajua hilo, katika mfano. Kama ukifundisha mifano, basi daima utakuwa sahihi, nafikiri, katika—katika mfano.

³¹⁰ Sasa, Yusufu, wakati alipozaliwa, yeye alichukiwa na ndugu zake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa nataka kuwaonyesha, Yusufu anawakilisha Kanisa lililojazwa na Roho. Yusufu alichukiwa na ndugu zake. Kwa nini? Kwa sababu alikuwa ni wa kiroho. Yusufu asingeweza kujiepusha kwa sababu angeweza kuona ono. Asingeweza kujiepusha kwa sababu aliota ndoto, mnaona, na angeweza kufasiri ndoto. Yeye, hicho ndicho kilichokuwa ndani yake. Asingeweza kuonyesha kitu kingine chochote ila kile kilichokuwa ndani yake. Vema, basi, ndugu zake wakamchukia, bila sababu. Lakini baba yake alimpenda, kwa sababu baba yake alikuwa ni nabii.

³¹¹ Mnaona jinsi ilivyokuwa kwa Yesu? Mungu alimpenda Mwanawe. Lakini hao ndugu, hao Mafarisayo na Masadukayo, walimchukia, kwa sababu angeweza kuwaponya wagonjwa, na kutabiri mambo, na kuona maono, kufasiri. Mnaona ninalomaanisha? “Walimchukia, pasipo sababu.”

³¹² Nao walifanya nini na Yusufu? Walijifanya alikuwa amekufa, nao wakamtupa shimoni. Wakachukua koti lililojaa damu, la rangi saba, ambalo baba yake . . .

³¹³ Kuna rangi saba tu katika upinde wa mvua. Nao upinde wa mvua, tunajua ni nini, ambao tutaufikia baadaye kidogo, nafikiri, usiku wa leo. Upinde huu wa mvua juu Yake hapa, Yesu, ambapo, “Alionekana kama jiwe la yaspi na akiki, na upinde wa mvua.” Upinde wa mvua ni agano.

314 Na hilo lilikuwa ni agano la Mungu juu ya Yusufu. Ndipo wakapaka koti lake damu, wakampelekea baba yao. Naye alidhaniwa kwamba amekufa. Na . . .

315 Lakini yeye alitolewa shimoni na kuwekwa kwenye—kwenye. . . akauzwa kwa Farao, mtu fulani huko Misri, na je—jemadari akamweka. Nao walipofanya hivyo, yeye, jambo baya likainuka dhidi yake, nao wakamtupa gerezani. Na huko akatabiri, na kuwaambia watu wawili ambapo mmoja angeenda na ambapo huyo mwingine angeenda; mnyweshaji na—na mwokaji, kulingana na ndoto zao.

316 Kisha akainuliwa kutoka huko, akapelekwa kwenye mkono wa kuume wa Farao. Basi hakuna mtu angaliweza kumgusa Farao, ila tu kupitia Yusufu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

317 Hili sasa. Sasa, ninii. . . hapo Yusufu basi alipouzwa huko kwa Wamisri. Basi, angalieni, kila kitu alichofanya kilimwainisha Kristo. Mwangalieni huyu mnyweshaji na mwokaji mle ndani, nao wote wawili waliota ndoto. Naye Yesu, alipokuwa kwenye nyumba Yake ya gerezani. Kumbukeni, Yusufu alikuwa gerezani. Naye Yesu alipokuwa kwenye gereza Lake, (vipi?) ameangikwa msalabani, kulikuwako na mmoja aliyeokolewa na mwingine aliyepotea. Yusufu, alipokuwa katika gereza lake, mmoja aliokolewa, mwingine akapotea.

318 Pia angalieni. Ndipo baada ya Yesu kuondolewa msalabani, Yeye aliinuliwa Mbinguni, na ameketi kwenye mkono wa kuume wa yule Roho mkuu, Yehova. “Hakuna mtu awezaye kumjia Mungu ila kwa njia Yangu.” Hakuna *Salamu Maria*, hakuna heri *huyu* ama heri *yule*. Lakini, kwa Yesu Kristo, “Mpatanishi pekee aliyepo kati ya Mungu na wanadamu,” ule mwili wa thamani ambamo Mungu alifanyia maskani, miongoni mwetu, ambaye alilichukua Jina la Mungu. Naye Mungu akachukua jina la kibinadamu. Mungu alichukua . . .

319 Angalieni hapa. Hapo mwanzo, wakati Adamu. . . Kamwe siwezi kuliondokea hilo. Inaonekana kana kwamba mtu fulani halipati, mahali fulani. Angalieni. Hapo mwanzo. . . Hebu niwaonyeshe jambo fulani tena. Roho Mtakatifu ananionya nifanye hivi. Ninaliacha somo langu kwa dakika moja. Wakati habari za kwanza zilipofika Utukufuni, ya kwamba yule mwana alikuwa amepotea, Adamu, je, Mungu alimtuma Malaika? Je, alimtuma mwana? Je, alimtuma mtu mwingine yeyote? Yeye alikuja, Mwenyewe, kumkomboa mwanawe aliyepotea. Haleluya! Mungu hakuliaminisha mtu mwingine ila Mwenyewe. Mungu alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu, na kumkomboa mwanadamu, Mwenyewe. Ni. . . “Tumeokolewa,” Biblia ilisema, “na Damu ya Mungu.” Mwanadamu, Mungu alikuwa. . . Mungu asiyepatikana na mauti alifanyika mtu, apate kuondoa dhambi, kuwa Mwana-Kondoo,

Mwenyewe; kuingia Utukufuni, ametiwa utaji, na Damu Yake Mwenyewe mbele Zake, ng'ambo ya pazia.

320 Sasa, Yusufu, huyo anaenda Misri. Na huko aliinuliwa kutoka gerezani mwake, hata kwenye mkono wa kuume wa Farao, naye akafanywa msimamizi. Basi kila kitu kilifanikiwa katika siku za Yusufu.

321 Sasa, Yesu atakaporudi, hata jangwa litanawiri kama ua. Yeye ni Mwana wa ufanisi, mfano wa Yusufu.

322 Walimweka Yusufu katika . . . Jemedari alimweka nyumbani mwake; kila alichofanya, alifanikiwa. Walimweka gerezani, na gereza lote likafanikiwa. Kila walichofanya, alifanikiwa. Na wakati alipoinuliwa, cheo cha juu zaidi, cha Farao, halifa wa Farao, kila kitu huko Misri kilifanikiwa zaidi ya chochote kile ulimwenguni.

323 Atakaporudi, itakuwa ni nchi ya ufanisi. Majangwa ya kale yatachanua, na kutakuwako na chakula kila mahali. Nasi tunaweza, kila mmoja, kuketi chini ya mtini wetu wenyewe, na kucheka na kushangilia, na kuishi milele Uweponi Mwake, hapo atakapokuja kama Mfalme.

324 Yeye alikuwa ni Mwana wa Adamu, Nabii. Amina. Alikuwa ni Mwana wa Adamu, Dhabihu, Kuhani. Yeye ni Mwana wa Adamu, kama Mfalme, Mwana wa Daudi akiketi kwenye kiti cha enzi cha ukuu Wake. Mwana wa Adamu, Yeye ni dhi- . . . Mungu aliyedhihirishwa kama Mwana wa Adamu. Alishuka akawa mtu, apate kuziondoa dhambi ulimwenguni. Alifanyika mwanadamu, kama Nabii. Akafanyika mwanadamu, kama Kuhani. Alifanyika mwanadamu, kama Mfalme; Mfalme wa Mbinguni, Mfalme wa watakatifu, Mfalme wa Milele; daima alikuwa ni Mfalme, daima atakuwa Mfalme, Mfalme wa Milele.

325 Sasa angalia, basi, Yusufu. Kabla Yusufu hajaondoka, iliwabidi kupiga baragumu, kwanza. Nao watu wakapiga makelele, "Mpigieni Yusufu magoti." Haidhuru mtu alikuwa akifanya nini, alikuwa akiuza bidhaa mtaani, parapanda hiyo ilipolia, aliinamisha goti lake. Mtu alikuwa tayari tu kunyosha mkono wake kuchukua pesa zake, bali aliinamisha goti lake, Yusufu alikuwa yuaja. Loo! Ninii. . . mwi—mwi—mwigizaji alikuwa tu tayari kuanza mchezo wake, naye angefanya nini? Ilibidi akome. "Yusufu yuaja." Parapanda ililia.

326 Moja ya siku hizi, kila kitu, hata wakati, utasimama kimya. "Parapanda ya Mungu itakapolia, nao waliokufa katika Kristo watafufuka, na ile asubuhi itapambazuka Milele, angavu na nzuri." Kila kitu kitainamisha goti. "Kila goti litainama, na kila ulimi utakiri Hilo."

Anza sasa. "Dhambi za watu wengine huwatangulia, wengine zinawafuata."

327 Lakini sasa angalia kilichotukia. Ni tukufu jinsi gani! Wakati Yusufu basi... baada ya kumwoa Mmataifa na kupata familia, Efraimu na Manase, wanawe. Hivi uliona mwishowe? Wakati Yusufu... Yakobo alipoanza kuwabariki Efraimu na Manase. Alipoanza kuweka mikono yake, alimweka Efraimu mkono wa kuume, Manase mkono wa kushoto, kumpa baraka za mkono wa kuume aliye mkubwa zaidi. Lakini alipoanza kuomba, mikono yake ikapitana, naye akampa aliye mdogo zaidi baraka za mkono wa kuume badala ya yule aliyekuwa mkono wa kuume.

328 Ndipo Yusufu akasema, "Sivyo, Baba." Kasema, "Umeweka baraka juu ya Manase badala ya Efraimu."

Naye akasema, "Mungu ameupitanisha mkono wangu."

329 Ati nini? Kutoka kwa Wayahudi, yule mkubwa zaidi, wa kwanza kuchaguliwa na Mungu, kupitia kwa Msalaba zilikuja baraka zikawarudia Mataifa, kumpata Bibi-arusi. Baraka zilikuja kupitia Msalaba, kutoka kwa Myahudi hadi kwa Mmataifa. Walikataa, waliukataa Msalaba, kwa hiyo Yeye akamchukua Bibi-arusi wa Mataifa.

330 Sasa wakati Yusufu, kabla ya jambo hili, wakati alipokuwa... aliposikia habari za ndugu zake, ambao... Walikuwa nje ya ushirika kwa muda wa miaka mingi, hao Wayahudi.

331 Sasa angalieni. Tunarudi kwa Zekaria sasa, ambako wanalia kwa huzuni, na kuomboleza na kulia kwa huzuni. Na hata jamaa watajitenga na jamaa zingine, watoke, waseme, "Tulifanyaje jambo hilo? Tungewezaje kamwe kufanya hilo?" Wakati wanaposema, "Ulipata wapi makovu hayo, alama hizo mikononi Mwako?" hata wale waliomchoma. "Atakuja katika mawingu. Nao watamwona, hata wale waliomchoma. Na kila nyumba itaomboleza, nao watalia." Hawatajua la kufanya.

332 Na wakati Yusufu... Mnajua hadithi hiyo. Wakati alipowaona ndugu zake, naye akajifanya kana kwamba asingeweza kuzungumza Kiebrania, na akamleta mtafsiri kumtafsiria. Wala asingeweza kuzungumza Kiebrania, alijifanya; bali alitaka kujua. Na kwa hiyo wakati hatimaye, siku moja, walipomleta ndugu yake mdogo, je, mliona? Benyamini ndiye aliyeichochea nafsi ya Yusufu?

333 Ni kitu gani, siku hizi, kitakachoichochea nafsi Yake, Yusufu wetu, Yesu? Lile kanisa dogo ambalo limekuwa huko Irani, ambalo limeshika amri za Mungu. Na ni watu waliozaliwa upya ambao wamekusanyika Palestina, na kurejeshwa tena. Ile Nyota yenye ncha sita ya Daudi, bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni, taifa limezaliwa katika miaka michache iliyopita. Hiyo hapo Israeli.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
 Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
 Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
 na hofu;
 Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.
 Siku ya Ukombozi imekaribia,
 Mioyo ya watu inazimia kwa hofu; (Hebu
 liangalieni tu, wote wamekuwa wazimu.)
 Jazweni na Roho, taa yenu imetengenezwa na
 ni safi,
 Tazameni juu, ukombozi wenu umekaribia.
 Manabii wa uongo wanadanganya, Ukweli wa
 Mungu wanaukana,
 Ya kwamba Yesu aliye Kristo ndiye Mungu
 wetu;
 (Utukufu! Lakini Ufunuo umekuja.)
 Kwa hivyo tunatembea ambapo mitume
 wamekanyaga, (Mahali pao pale pale.)
 Kwa kuwa Siku ya Ukombozi imekaribia,
 Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
 Jazweni na Roho wa Mungu, taa yenu
 imetengenezwa na ni safi,
 Tazameni juu, ukombozi wenu umekaribia.

³³⁴ Loo! Loo, Yusufu, wakati alipomwona maskini Benyamini mdogo amesimama pale! Huyu ni ndugu yake mdogo. Mnamwona maskini Benyamini mdogo sasa juu...?... huko ng'ambo, ameketi kule? Makabila ya—ya dunia, ya Wayahudi, wamerudi kule ambako kutakuwako na mia moja arobaini na nne elfu wamesimama kule, kumpokea Kristo wakati watakapomwona Yeye Akija. Watasema, “Lo, huyu ni Mungu wetu Ambaye tumemngojea.” Ndipo wataona ninii iliyochoywa... “Haya yalitoka wapi?”

Akasema, “Katika nyumba ya rafiki Yangu.”

³³⁵ Nao wataomboleza na watalia. Na kila jamaa, makabila yao ya Daudi na Naftali na wote, watajitenga, kila jamaa, na kuomboleza wenyewe watakapomwona amesimama hewani, Yule waliyemchoma.

³³⁶ Ujumbe Wake utakuwa nini? Angalieni yale aliyosema Yusufu. Wakati aliposema... .

³³⁷ Angalieni jambo lingine. Wakati Yusufu alipowaleta hao watoto mbele zake, yeye aliwaangalia, akamwona maskini Benyamini. Akamwona Efraimu, akawaona hao wengine pale, wa Gadi na hao wote. Na yale makabila kumi na mawili, makabila kumi wakati huo, wamesimama mbele zake. Aliwaona wote wamesimama pale. Alijua walikuwa ni ndugu zake. Ndipo akamwangalia maskini Benyamini mdogo, moja kwa moja, koo lake likianza kufurika. Alijua walikuwa ni wake. Yeye alisema

nini? “Kila mtu na aniache.” Ilikuwaje kwa mke wake na watoto? Waliingia katika ikulu.

³³⁸ Kanisa la Kimataifa litaenda wapi kwenye Unyakuo? Katika Ikulu. Bibi-arusi, Haleluya, Bibi-arusi ataondolewa duniani, katika Unyakuo. Basi wakati Yeye atakaporudi, Bibi-arusi Wake hayuko wakati anapojitambulisha Mwenyewe kwa ndugu Zake, Wayahudi, wale waliomchoma, wale waliomkataa.

³³⁹ Lakini mke wake na wapendwa wake, marafiki wake wa karibu pale, we—wenziwe waliotumwa na Mungu walikuwa hekaluni. Ndipo alipoangalia, alisema walikuwa . . . Hawakujua. Walisema, “Loo, mtawala huyu mkuu!” Wakaanza kuambiana, mmoja kwa mwingine, loo, kuhusu mambo haya jinsi walivyofanya.

³⁴⁰ Ninaamini ilikuwa ni Efraimu, ama sio Efraimu, bali nasahau ilikuwa ni yupi sasa, ambaye—ambaye alisema, “Vema, hatukupasa kumwua ndugu yetu, Yusufu.” Kasema, “Mnaona, tunapatilizwa.” Rubeni, Rubeni alisema, “Hatukupasa kumwua ndugu yetu,” kasema, “kwa sababu, mnaona, tunapatilizwa kwa ajili ya yale tuliyoifanya.”

³⁴¹ Naye Yusufu akisimama pale; hawakufikiria angeweza kuelewa Kiebrania. Lakini alikijua.

³⁴² Wengine wanafikiria, hawezi kuzungumza . . . kuelewa kunena kwa lugha, lakini Yeye anajua yote kuihusu. Naam, Yeye anajua. Ufalme wa Kimataifa ulikuja pamoja na kunena kwa lugha na kufasiri, katika kichwa cha dhahabu (kichwa cha kwanza) kabla haujaanguka. Ni kitu gani kilichomaliza kipindi hicho cha kwanza cha wakati wa Mataifa? Maandiko ya mkono ya lugha zisizojulikana ukutani, na mtu pale ambaye angeweza kuzifasiri na kusema zilikuwa ni nini. Unaondoka vivyo hivyo. Amina. Uliingia na unaondoka vivyo hivyo.

³⁴³ Walidhani asingeweza kuelewa hizo lugha walizokuwa wakizungumza, bali alizijua. Wakasema, “Mnaona kile tumepata?”

Ndipo Yusufu akaona basi wanajutia yale waliyokuwa wamefanya.

³⁴⁴ Sasa Yeye anaona masikitiko yao na majuto kwa ajili ya kumkataa Yeye, kwa hiyo Yeye anafurika kwenye koo Lake sasa. Yuko tayari kuliondosha Kanisa Lake duniani, alipeleke Utukufuni. Kisha arudi, na ndipo makabila yote ya dunia yataomboleza.

³⁴⁵ Walifanya nini? Rubeni, hao wote, walianza kulia, wakasema, “Loo! Loo!” Walihofia na kusema, “Huyu ndiye. Sasa tunajua tutajuta. Sasa atatuua. Sasa yeye . . . Tunajua tutaangamizwa sasa hivi, kwa sababu huyo ni Yusufu ambaye ametuacha muda mrefu sana. Huyo ni Yusufu, ndugu yetu, sasa tutajuta kweli.”

346 Akasema, “Msijikasirikie. Mungu alifanya jambo hili apate kuhifadhi uhai.”

347 Mungu alifanya nini? Kwa nini Wayahudi wakamkataa Yesu? Kusudi sisi Wamataifa, ili, kwamba, watu aliowaita kwa ajili ya Jina Lake, Mungu alifanya hivyo kuhifadhi uhai wa Kanisa la Wamataifa, Bibi-arusi.

348 Makabila yote yaliyomkataa yataomboleza. Watajificha katika matundu, na katika miamba, na kadhalika, wakisema, “Tufiche, tuangukie, enyi milima.” Walilikataa, Yeye. Jamii zote za dunia zitaomboleza kwa sababu Yake. Na kila jamaa katika Israeli kule itajitenga. Jamaa zitajitenga, moja kwa nyingine, wakisema, “Ni kwa nini tukafanya hivyo? Tulimkataaje? Vipi? Yule pale amesimama. Yule pale Mungu ambaye tumemngojea. Na Yule pale, akiwa na alama za misumari mikononi Mwake, nasi tulifanya hivyo.”

349 Hivyo ndivyo hao ndugu walivyosema hasa moja kwa moja kule, waliporudi na kusema, “Yule pale Yusufu, tuliyemuza.”

Yeye alisema, “Mimi ni Yusufu, ndugu yenu, mliyeniua Misri.”

350 “Loo!” Waliogopa. Nao walikuwa wakiomboleza na kulia kwa huzuni, na kukimbiliana, “Tufanye nini?”

351 Akasema, “Msijikasirikie, maana Mungu alifanya haya yote. Mungu alinitanguliza.”

352 Mungu aliumba watu wote; watu weupe, watu weusi, wa hudhurungi, wa manjano, kila mtu. Mungu alimwumba kila mtu. Alimwumba Mmataifa, alimwumba Myahudi. Aliwaumba wote. Yote ni kwa ajili ya utukufu Wake. Nao Wayahudi ilibidi wakataliwe kusudi amchukue Bibi-arusi wa Kimataifa.

353 Hiyo ndiyo sababu ya mifano hii yote. Kusudi Bibi-arusi wa Kimataifa na ukoo Wake pamoja Naye, lile Kanisa tukufu la kipentekoste lililoosha katika Damu ya Mwana-Kondoo, huku nguvu zote za ufufuo zikiishi ndani yao, litapaa siku moja katika Unyakuo (kwa dakika moja, kufumba na kufumbua) waende kuwa Uweponi mwa Yesu, wakati Yeye akirudi (na kuondoa kila kitu) apate kujitambulisha Mwenyewe kwa ndugu Zake.

354 Angalia yale Maandiko yanayosema hapa, katika kufunga. Loo!

*Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona,
(sasa ananena kuhusu Kuja mara ya pili, sio Unyakuo),
na hao waliomchoma: . . .*

355 Mlango wa 7, kifungu cha kwanza . . . Ama, kifungu cha 7 cha mlango wa kwanza.

*. . . na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma:
na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake.
Naam, Amina.*

356 Ndipo anatoa ile nukuu mashuhuri. Ni nani Huyu? Ni nani Huyu wanayepaswa kwenda kumtafuta?

Mimi ni Alfa na Omega, Mimi ni A na Z, (A na Z za Kiyunani, alfabeti za Kiyunani). . .

357 Matendo 2:36, ninii. . . Petro alisema, “Hakuna jina jingine walilopewa chini ya Mbingu liwapasalo wanadamu kuokolewa kwalo.” Ama, la, samahani; ninalinukuu vibaya. Alisema, “Basi nyumba yote ya Israeli na ijue yakini, ya kwamba Mungu amemfanya Yesu yuyu huyu, mliyemsulubisha, kuwa Bwana na Kristo pia.”

358 Yohana 14:7 na 12, Tomaso alisema, “Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha.”

359 Kasema, “Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue?” Kasema, “Aliyeniona Mimi amemwona Baba. Basi wewe wasemaje, ‘Unionyeshe Baba?’ Mimi na Baba Yangu ni Mmoja.”

360 Nilisema hayo wakati mmoja kwa mtu fulani. Huyu mama akasema, “Hebu kidogo, Bw. Branham.” Kasema, “Wewe na mke wako ni mmoja, pia.”

Nikasema, “Lakini si wa namna hiyo.”

Akasema, “Samahani.”

Nikasema, “Je, unaniona mimi?”

Akasema, “Nakuona.”

Nikasema, “Je, unamwona mke wangu?”

Akasema, “Hapana.”

361 Nikasema, “Basi, Wao ni wa namna nyingine. Yeye alisema, ‘Ukiniona Mimi, umemwona Baba.’” Kwa hiyo hilo lilitosha.

362 Kwa hiyo katika Yohana Mtakatifu, ama Yohana wa Kwanza 5:7 hadi 8, ninyi nyote mnaoyaandika. Yohana wa Kwanza 5:7 hadi 8, Biblia ilisema. Mnenaji huyu, mtu yule yule aliyeuandika Ufunuo huu ambao Yesu alimpa, alisema, “Wako watatu washuhudiao Mbinguni: Baba, Neno (hilo Neno ni Mwana). . . Baba, Neno, na Roho Mtakatifu, na hawa watatu ni mmoja. Wako watatu washuhudiao duniani: maji, Damu, na Roho, nao hupatana; si mmoja, bali wanapatana kwa habari moja.”

363 Huwezi kuwa na Baba pasipo kuwa na Mwana. Huwezi kuwa na Baba au Mwana pasipo kuwa na Roho Mtakatifu. Kweli. Lakini wewe. . . Na maji, Damu, na Roho, hizo ni elementi zinazohitajika kuingia Mwilini Mwake.

364 Wakati kuzaliwa kwa kawaida kunapotukia, kitu cha kwanza kinachotukia wakati mwanamke anapomzaa mtoto mchanga ni kipi? Kitu cha kwanza, ni maji. Kitu cha pili, ni damu. Hiyo ni kweli? Kinachofuata, ni roho. Mtoto huyo mchanga anashika pumzi yake, anaanza kupumua. Maji, damu, na roho, hivyo ndivyo vinajumuisha kuzaliwa kwa kawaida.

365 Pia, Kuzaliwa kiroho. Ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo; kuhesabiwa haki kwa imani, kumwamini Bwana Yesu Kristo. Maji! Kinachofuata ni nini? Damu; kutakaswa, kusafishwa, kumtoa nje.

366 Hapo ndipo ninyi Wanazarayo mlipokosea; mlienda tu umbali huo wala hamkuenda mbele zaidi. Chombo kilichotakaswa madhabahuni, tayari kwa matumizi, bali hakitumiki. “Heri wao,” zile heri, “wenye njaa na kiu ya haki, kwa maana watajazwa.” Chombo kimetakaswa. Hiyo ni kweli.

367 Hiyo ni kama bikira. Neno *bikira* linamaanisha “safi, mtakatifu, asiyeghoshiwa, aliyetakaswa.” Watano walikuwa na mafuta, na watano hawakuwa nayo; watano walikuwa wamejazwa, na hao wengine walibaki tu katika utakaso. “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mliipoamini,” ninyi Wabaptisti, Wapresbiteri?

“Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu yeyote.”

“Basi, mlibatizwaje?” Uh-huh.

368 Baada ya kuweka mikono yake juu yao, walimpokea basi, wakiisha kuokolewa na kutakaswa, walijazwa na Roho Mtakatifu. Kweli.

369 Maji, Damu, Roho! Yesu alikuja kuosha na kusafisha, na kulitakasa Kanisa, apate kuja na kuishi ndani. Kwa Damu Yake Mwenyewe; Yeye alitoa Damu Yake Mwenyewe iliyozaliwa na Mungu, apate kutusafisha na kuzaliwa kwetu kwa kujuana kimwili, na kutupa chombo kilichotakaswa, kitakatifu ili kwamba Yeye Mwenyewe apate kuja.

370 “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona kwa kuwa Mimi,” kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ukamilisho.” Amina. “Kote kote, nitakuwa pamoja nanyi na ndani yenu. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mungu ndani ya Kanisa! Loo, jamani! Uungu! “Wako watatu washuhudiiao Mbinguni: Baba, Neno (Mwana), Roho Mtakatifu. Hao ni Mmoja.”

371 Sasa, unaweza kuokolewa bila kutakaswa. Unaweza kutakaswa na usiwe na Roho Mtakatifu; kweli, roho iliyotakaswa, bila ya kujazwa. Kuutakasa moyo wako, kuusafisha moyo wako, pasipo kuujaza na kitu fulani. Hivyo ndivyo Yeye alivyosema, “Roho mchafu amtakapo mtu, hutembea mahali pasipo maji. Anarudi, anakuta nyumba yake imepambwa kabisa, naye anaingia. Hali ya mwisho ya mtu huyo ni mbaya mara nyingi, mara saba, kuliko ilivyokuwa kwanza.”

372 Hilo ndilo lililowapata ninyi Wapilgrim Holiness, Wanazarayo, na kadhalika. Mlikubali. Ndipo wakati Roho Mtakatifu alipokuja, akaanza kunena kwa lugha, na kutoa ishara na maajabu, mlimwita “ibilisi” na mkazikufuru kazi za

Mungu, mkaziita “kitu kichafu.” Basi mnaona mahali kanisa lenu lilipoelekea? Ondokeni kwake! Ile saa imewadia, Ufunuo wa Yesu Kristo unafundishwa, Mungu akifunuliwa katika nguvu za madhihirisho Yake ya Roho Mtakatifu. Amina. Siku ya ukombozi imekaribia.

373 Sasa, Uungu ndani Yake, Timotheo wa Kwanza 3:16.

...bila shaka siri ya uungu ni kuu: kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, . . . akaonekana na malaika, . . . akaaminiwa katika ulimwengu, akachukuliwa juu katika utukufu.

374 Loo, kuendelea tu na kuendelea na kuendelea. Lakini tuko wapi sasa? Mwishoni mwa kifungu cha 8.

375 Usiku wa leo tunaanza ki—kifungu cha 9, *Ono La Patimo*. Loo, kuna mambo makuu tuliyowekewa akiba. Je, mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

376 Mnampenda kweli? Je, Mungu amejitambulisha Mwenyewe kwenu, amefunuliwa kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, apate kuondoa dhambi? Anajifunua Mwenyewe katika siku hizi za mwisho katika makanisa Yake, akijifanya Mwenyewe ajulikane.

377 Sasa, mambo yaya haya yanayoendelea Kanisani, angalieni muone, mwishoni mwa Ujumbe huu, kwamba ikiwa Biblia haisemi mambo haya yatatukia, vivyo hivyo hasa. Angalieni kama hayakutukia vivyo hivyo kabisa, katika Wakati wa Efeso, na wa Pergamo, Thiatira, na kuendelea, kila wakati.

378 Ikasema jinsi ambavyo Luther angefanya, na jinsi Wesley angefanya. Na jinsi dhehebu hili la Pentekoste litakavyoingia katika Laodikia, hali ya uvuguvugu, lakini, katikati ya hayo, Yeye angewavuta watu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Tuko mwisho. Loo, nina furaha sana! Na, loo, kama nilivyojiona mwenyewe nikiondoka, na kuwaangalia marafiki zangu na kadhalika, na kuona ulimwengu na—na machafuko yaliyomo, halafu kuwazia ya kwamba Kuja kwa Bwana kunakaribia sana. Tuko kwenye mwisho wa wakati.

379 Mioyo ya watu inazimia kwa hofu. Kila mahali, kila mtu, inatisha sana kwenye redio, wakati wote, “Iweni tayari kwa uvamizi wa angani. Ingizeni *hiki*, ingizeni *kile*, kisha mshuke mwingie kwenye chumba cha chini ya ardhi.” Mtajifichaje na hiyo? Hamwezi kujificha kutoka kwa hiyo. Vema, kitu hicho kitaingia futi mia moja na hamsini ardhini, kwa yapata maili mia moja na hamsini, mraba. Mbona, mtikiso wake mkali ungeninii . . . Kama ikianguka hapa, ingetikisa Indianapolis

ianguke chini. Mbona, ingeulipua tu Indianapolis vipande-vipande, igonge papa hapa Louisville, mnaona, moja ya hizo. Ni vigumu kusema wana kitu gani mbali na hiyo.

³⁸⁰ Pia, angalieni, haiwabidi kuninii. . . Mnajua, haiibidi Urusi kufanya hivyo. Kyuba inaweza kufanya hivyo. Mahali popote padogo sana, mahali pa—padogo sana kama Alkatrazi huko ng'ambo, pangeweza kufanya hivyo, kuufunika ulimwengu mzima. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kulenga shabaha na kuvuta kamba moja. Hamhitaji jeshi lolote. Mnahitaji mwendawazimu mmoja tu kufanya hivyo, aliye mikononi mwa ibilisi. Hiyo ni kweli kabisa. Angefanya hivyo, na ndipo kitu hicho chote kimekwisha. Kimekwisha basi.

³⁸¹ Lakini, loo, hebu niwape kitu hiki kilichobarikiwa. Tunapoona limekaribia hivi, tunapoona kwamba lingetukia kabla ya mapambazuko. Kumbukeni, Kanisa linaenda nyumbani kabla jambo hilo halijatukia. Unyakuo unatukia kabla ya hapo.

³⁸² Sasa, msije mkachanganyikiwa, kumbukeni, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kama ilivyokuwa katika siku za Lutu.” Kumbukeni, kabla mvua yoyote haijanyesha, Nuhu alikuwa ndani ya safina. Mnaona? Nuhu alikuwa ndani ya safina. Alibebwa juu, kupitia haya. Na sasa, Nuhu alikuwa ni mfano wa Myahudi. Bali Henoko alienda nyumbani bila kufa. Ndipo Nuhu alipomwona Henoko akienda, alijua wakati ulikuwa umewadia, akaanza shughuli za safina. Hiyo ni kweli. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Nuhu, wakati Henoko alipoenda nyumbani. Na mara Kanisa la Kimataifa likiondolewa, ndipo Yeye anajitambulisha kwa Israeli. Mnaona? Hiyo ni kweli.

³⁸³ Kumbukeni, katika siku za Lutu, kama Yesu alivyosema, kabla chembe moja ya moto kuipiga nchi, yule Malaika alisema, “Hima. Harakisha. Ondoka mahali hapa, kwa kuwa siwezi kufanya lolote mpaka umekuja huku.” Kabla moto wowote kushuka, Lutu na familia yake walikuwa wametoka na kwenda. Kwa hiyo, Unyakuo utakuja kabla ile Dhiki haijaingia.

³⁸⁴ Ie Dhiki, watu wengi huzichanganya. Tutainyosha, juma hili, Bwana akipenda, kwa msaada wa Bwana. Kumbukeni, mnatazamia Wakati mkuu wa Dhiki, huo ulikuwa, kama mtaufananisha huo katika Biblia, huo ulikuwa ni siku za Taabu yake Yakobo, mnaona, wakati alipotaabika. Huo haukuwa na uhusiano wowote na Mataifa. Mataifa hawana uhusiano wowote nao. Hakuna mfano wa hayo katika Biblia. Kanisa la Wamataifa Limenyakuliwa.

³⁸⁵ Nanyi mnatazamia “maji kugeuka kuwa damu,” na vitu kama hivyo. Hilo linatokea huko kwa Israeli tena, huko nyuma pamoja na Musa na Eliya, hapo watakaporudi. Eliya, kwa mara ya nne, anarudi katika roho. Hakuna mmoja wa hao aliyekuwa amekufa.

386 Ama, ninii...Musa alikufa; hawakujua mahali walipomzika. Ilimbidi kufufuliwa mahali fulani kati ya hapo na kule, maana, kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, huyo hapo amesimama, akizungumza na Yesu. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona?

387 Kwa hiyo watarudi na kuuawa, na kulala kwenye mtaa wa kiroho unaoitwa "Sodoma," ambapo Bwana wetu alisulubiwa, Yerusalemu. Watakuwa wakiwahubiria Wayahudi, na kuipiga nchi, na kuzifunga mbingu, na kadhalika namna hiyo. Na mwisho wa huduma ya Wamataifa utaendelea na kuungana na hiyo, nao Wamataifa wataenda nyumbani, nayo huduma hiyo itaendelea. Kutakuwako na maangamizi ya vitu vyote. Theluthi mbili ya dunia ilianguka, na kila kitu kingine. Wakati miili hiyo iliyokufa ilipolala kule mitaani, siku tatu, angalieni ilikuwa ni ya namna gani.

388 Angalieni picha hizi nilizopata kutoka huko Marekani ya Kusini, wakati walipomwua yule mmishenari wa Kipentekoste kule, mke wake, wamelala mtaani, naye pamoja na watoto wawili wadogo. Msichana mdogo, na maskini tumbo lake limevimba namna *hiyo*. Hata wasingewazika. Wakatembea pale, wakaitemea mate namna hiyo, kwa muda wa siku tatu ama nne. Ndugu Kopp aliipiga hiyo picha. Ninazo nyumbani, mnaona, jinsi wanavyofanya.

389 Ndipo watapelekeana zawadi, wao kwa wao. Angalieni jinsi hilo linavyoainishwa katika Biblia, muone ni kanisa gani litakalofanya jambo hilo. Hiyo ni kweli, imekaribia kabisa, na linaingia moja kwa moja ndani kama nyoka sasa hivi, janja tu liwezavyo kuwa, ishara ya mambo sasa hivi.

390 Angalieni unabii Bwana alionipa mwaka wa '33, jinsi lingetendeka, "Wangewaruhusu wanawake kupiga kura. Katika kupiga kura, wangemchagua mtu asiye faa." Mambo saba yalitolewa, na matano ya hayo tayari yametukia. Jambo lililofuata lilikuwa ni mwanamke mashuhuri, kanisa, mamlaka ama kitu fulani, angeichukua Marekani hii, kutawala. Kisha nikaiona tu kama majivu, imelala, ambapo ilifikia mwisho wake. Ilikuwa ni wakati wa mwisho.

391 Lilisema, "Wangukuwa na mtambo ambao ungejiendesha. Haikuwabidi kuwa na dereva ndani yake." Ndio kwanza waukamilishe. Lilisema, miaka kumi na mmoja . . .

392 Roho Mtakatifu aliniambia. Lile pale kwenye karatasi. Hamwezi . . . Haliwezi kukanushwa. Lile pale kwenye karatasi, kama vile Roho Mtakatifu alivyosema.

393 Miaka kumi na mmoja kabla ya ile Ngome ya Maginot kujengwa, nilisema, "Wajerumani . . . Marekani itaninii tu . . . Rais Roosevelt atakuwa ndiye mhuni wa hao wote." Na hiyo ni kweli. Alikuwa hivyo.

394 Sio kuwaudhi ninyi Wanademokrasia, bali ni—ninawaambia. Sio Mwanademokrasia wala Mripablikani sasa. Ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ambaye tunanena habari zake. Mimi si Mwanademokrasia wala Mripablikani. Mimi ni Mkristo. Kwa hiyo basi, hao, vyovyote ilivyokuwa, lakini angalieni pale.

395 Basi angalieni hapa, hivi majuzi, kama mkitaka kuona jinsi hilo lilivyo kundi la mahaini. Kuchukua mitambo hiyo na kuikarabati, ambapo, kila mara ungempigia kura Bw. Nixon, ilikubidi kumpigia jamaa huyu mwingine, wakati uo huo. Ed- . . . J. Edgar Hoover aliifichua mitambo hiyo. Ni wangapi wamekuwa wakisoma hayo? Mbona, hakika, yamejaa kwenye magazeti yote, habari, na kila kitu kingine. Mnaona mahali tulipo?

396 Hakuna kitu kilicho kiaminifu tena ila Kristo. Amina. Loo, Kitabu hicho cha kale kilichobarikiwa! Hicho Ndicho. Hicho Ndicho pekee kinachokwambia wewe ni nani, unakotoka, na unakoenda (Naam, bwana.), ni Kitabu hiki kilichobarikiwa, loo, hilo hunifanya nimpende Yeye. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Imani katika Baba, imani katika Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, hawa watatu ni
Mmoja;
Pepo watatetemeka, na wenye dhambi
wataamka;
Imani katika Yehova hufanya chochote
kitikisike.

397 Amina. Ni siku kuu jinsi gani iliyo mbele zetu, enyi marafiki! “Ufunuo wa Yesu Kristo ambao Mungu alimpa malaika Wake, naye akaja na kumwonyesha Yohana, ipate kujulikana kote katika Nyakati za Kanisa, yale tuliyouwekewa akiba.”

398 Bwana na atubariki sasa, tunaposimama kwa miguu yetu. Na yeyote anayepiga piano, naomba utupe sauti ndogo tafadhali, *Peleka Jina La Yesu.*

399 Sasa sikilizeni. Kunao, hapana shaka, kunao wageni hapa miongoni mwetu maskanini asubuhi ya leo. Ninawatakeni muwape mikono. Waalikeni, waende nyumbani pamoja nanyi, na kadhalika. Na kumkaribisha kila mtu. Ninataka kila mtu ahakikishe amefanya hivyo.

400 Pia kumbukeni ibada itaanza saa moja, usiku wa leo. Na saa moja u nusu, nitakuwa nikizungumza juu ya *Ono La Patimo*. Kesho usiku, Bwana akipenda, nitakuwa nikizungumza juu ya wakati wa kwanza wa kanisa, Efeso, juu ya Wakati wa Kanisa.

401 Sasa tutaimba *Peleka Jina la Yesu*, maskini wimbo wa maskani yetu wa kupumukana. Basi hebu kila mtu aimbe sasa. Vema.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Peleka kila uendako.

Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Jina la thamani, Loo ni tamu
jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

⁴⁰² Sasa kabla hatujaimba ubeti unaofuata, ninawatakeni Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, Wakatoliki, Nazarayo, Pilgrim Holiness, wote wainyoshe mikono yao huku, upeane mikono na mtu aliye mbele yako, kando yako, nyuma yako, useme, “Msafiri Mkristo, rafiki, nina furaha kuwa pamoja nawe hapa asubuhi ya leo. Nina furaha kufanya ushirika pamoja nawe, kwenye mambo ya Mungu. Ninajua tumekuwa na wakati mzuri sana. Ninatumaini kukuona hapa tena usiku wa leo.” Kitu kama hicho, unapopeana mikono na watu, mbele yako, nyuma yako, karibu nawe.

Tukilisujudia Jina la Yesu,
Tuonane usiku wa leo, Ndugu Neville. Tuonane usiku wa leo.

. . . miguuni,
Mfalme wa wafalme, Mbinguni, tutamvika
taji,
Safari yetu itakapokamilika.

Loo Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Hata twonane! hata twonane!
Hata twonane miguuni pa Yesu; (hata
twonane,)

Hata twonane! hata twonane!
Mungu awe nanyi hata tutakapoonana tena!

Sasa tunapoinamisha kichwa chetu:

Hata twonane! hata twonane!



UFUNUO WA YESU KRISTO SWA60-1204M
(The Revelation Of Jesus Christ)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 4 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org